SUPA JACKPOT
TZS. 1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**MOI** yabuni mkono wa umeme kwa wenye ulemavu

UKURASA 5


Ukurasa 12
Janga la uraibu wa kamari linavyokuwa pasua kichwa

BUFE
IJUMAA AGOSTI 4, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Wamachinga Temeke sasa ni masoko tu waambiwa kuuzia barabarani ni kizamani
Ukurasa 12

Jicho la TAFORI viwanda vya bidhaa za misitu, ni kuviongeza mara dufu

•Jitihada kuhusu miti inayotoweka zaimarishwa

Na Christina Haule, MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), imeazimia kuongeza idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya misitu kutoka 650 hadi 1,500 katika kipindi cha miaka saba ijayo.

Ni baada ya kuweka mpango mkakati ambao utaimarisha huduma za misitu kwa jamii na kwamba hadi ifikapo mwaka 2030 viwanda hivyo vinatarajiwa kuongezeka na kuimarika ili kutoa ajira, kuchangia pato la taifa na kubadilisha maisha ya watanzania, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa TAFORI, Dk. Revocatus Mushumbusi.

Katika mahojiano ya Nipashe yanayofanyika mjini Morogoro, anasema katika mwaka wa fedha 2022/2030 taasisi inakusudia kufanya tafiti tano za kufanikisha kimkakati huo kwa lengo la kuboresha huduma za misitu kwa jamii ikiwamo kutathmini rasilimali za misitu na kuongeza tija katika viwanda vinavyotegemea malighafi kutoka misituni.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAFORI anasema taasisi imeweka mpango mkakati ambao utaimarisha huduma za misitu kwa jamii na kwamba hadi ifikapo 2030 viwanda vya kuchakata mazao ya misitu viwe vimeongezeka kutoka 650 hadi kufikia 1,500.

Anasema tayari wameshafanya tathmini ya viwanda hivyo ili kuvipatia malighafi kama inavyotakiwa ambapo tathmini ya awali imefanyika katika mikoa ya kusini na kubaini uwepo wa viwanda vya mazao hayo ya misitu kuwa ni 592 katika eneo hilo pekee.

Mkurugenzi Mushumbusi anasema viwanda hivyo 592 vya mikoa vinapatikana Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Rukwa na vinashughulika na kuchakata bidhaa zinazotokana na uhandisi wa mazao ya misitu, vingine vinatengeneza karatasi, kutengeneza mkaa mbadala na vya kuzalisha umeme.

Anasema viwanda hivyo vinapata malighafi kwa asilimia 95 kutoka kwenye mashamba ya misitu ya serikali na watu binafsi yaliyoko maeneo mbalimbali.

Anaongeza kuwa tathmini hiyo imebaini kuwa bado kuna uchache wa misitu inayohitajika katika kulisha viwanda hivyo ambapo viwanda 592 ili vifanye kazi ipasavyo vinapaswa kupata misitu yenye ujazo mita milioni 4.5 kwa mwaka wakati kiasi kinachopatikana kwa sasa ni milioni 1.5 kwa mwaka sawa na asilimia 34 pekee ya uwezo uliopo wa kuvilisha.

Anasema zipo hekta 207,320 ambazo zina miti wakati asilimia 75 ya miti hiyo yote ni jamii ya misindano.

Anatoa rai kwa wadau wa misitu kuona haja ya namna ya kuendelea kuanzisha mashamba ya kuzalisha miti ya kutosha ili kulisha viwanda 592 vilivyopo katika kanda moja ya kusini pekee ambayo ni ya awali wakati tafiti zikipangwa kuendelea katika kanda nyingine nchini.

Mkurugenzi huyo anasema pia TAFORI inafanya tafiti ya pili ambayo ni kutathmini mchango wa sekta ya misitu katika pato la taifa kwa kutumia utafiti wa kijani ambao mpaka sasa mchango wa sekta ya misitu katika pato la taifa ni asilimia tatu hadi nne.

Anasema utafiti huo uliofanyika mwaka 2021/22 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wa vyuo vikuu vya UDOM na Chuo kikuu cha Sokoine wakitazama vitu vinavyohusika na mazao ya misitu kama mbao, nguzo, mkaa, nta, samani na asali kwa lengo la kupandisha mchango wa sekta misitu.

Dokta Mushumbusi anasema pia utafiti mwingine ni kutathmini idadi ya miti, masoko na namna ya kuzalisha miti ambayo ipo hatarini kutoweka akitaja jamii za msandali, msekeseke na mkulungu.

Anasema miti jamii ya miseseke na mikulungu hutumika katika uzalishaji wa mbao za kiwango cha hali ya juu ya daraja la kwanza wakati msandali hutumika katika kuzalisha manukato.

Anafafanua kuwa miti hiyo imepungua sana kutokana na miti hiyo kuota katika mazingira ya misitu ya asili na uvunaji wake kufanyika kwa uharibifu sababu wanavuna kuanzia mizizi.

Dokta Mushumbusi anasema wataendelea na utafiti kujua kiasi cha miti iliyopungua na kiwango kilichobaki msituni na hali ya soko ikoje na mwisho wa yote watumie mbinu gani kuhakikisha wanazalisha miti hiyo ili kuziba pengo.

Anasema utafiti umewaongoza katika mikoa ya nyanda za juu kusini na kubaini kiasi cha miti kilichopo hakitoshi ambapo tayari wameanza kukusanya vipando vya maabara na bustanini na kuanza kupanda miti hiyo, kuitunza kwa nia ya kuifikisha kwenye mashamba.

"Kazi yetu kubwa katika miti yote ni kuhakikisha tunaizalisha kadri tunavyoweza kupata vipando vya kutosha na pengine ifike mahali tuweze kuvisambaza kwa wananchi na tufanikishe kuanzisha mashamba maalum badala ya kutegemea miti hiyo kuipata katika mashamba ya asili peke yake" anasema.

Hivyo, anasema utafiti umeonyesha kuwa ipo miti mingine yenye ubora unaofanana na hiyo ambayo bado haijatambulika zaidi kuweza kutumika na kuwa mbadala wa jamii hiyo inayotishiwa na hatari ya kutoweka.

Moja ya kiwanda cha kuchakata mazao ya misitu kilichopo mkoani Ruvuma, kinachosindika magogo ya mti wa msekeseke. PICHA: CHRISTINA HAULE


Inaendelea Uk 12

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Agosti 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581392
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Bosi benki, wanafamilia watatu wafa kwa ajali

• **Walikuwa** wanasafirisha maiti; yumo mhadhiri wa Mzumbe... *Endelea ukurasa 2*








Ndugu wanne wa familia moja (pichani), waliofariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria lenye namba za usajili T 104 CBU Toyota Prado kugongana uso kwa uso na Scania lori lenye namba za usajili T 881 DWU likiwa na tela namba T888DWU katika kijiji cha Mapatano, Kata ya Mbwewe, Wilaya ya Kipolisi Chalinze mkoani Pwani jana. Picha nyingine ni mabaki ya Toyota Prado baada ya ajali. **PICHA: MTANDAO**

## Serikali yaleta mwekezaji mpya mazao ya kilimo

UKURASA 4

UJENZI HOLELA

## NHC yashauri 'uswahilini' kubomolewe, kujengwe upya

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YATAMBA KUFANYA MAKUBWA** UK.24

**KATUNI** UK.6



Wataalam wa misitu kutoka nchi 13 za Afrika, wakipata maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja wa Msitu wa Olomotonyi wa Chuo Kikuu cha Sokoine Tawi la Arusha jana, kuhusu namna ya kufanya kilimo shirikishi ambapo wananchi wa vijiji vya jirani hupanda mazao kwenye shamba la miti kwa miaka mitatu huku wakipalilia miti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WIKI YA UNYONYESHAJI

# Kinababa waelimika waacha kunyonya maziwa ya wake zao

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Chakula na Lishe (TFNC), imesema vyombo vya habari vimesaidia kuelimisha jamii kuondokana na dhana potofu ya wanaume kutumia maziwa ya mama kama dawa ya kuongeza nguvu za kiume na kuondoa arosto ya pombe.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFNC, Dk. Germana Leyna, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waaandishi wa habari, kuhusu wiki ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama duniani, inayoanza Agosti Mosi -7, kila mwaka.

Kaulimbinu ya mwaka huu: 'Saidia Unyonyeshaji: Wezesha wazazi kulea watoto na kufanya kazi zao kila siku'.

"Mtakumbuka kuwa mwaka mmoja nyuma liliibuka suala la kinababa kupendelea maziwa ya watoto mlitusaidia sana (waandishi wa habari) kuelimisha kinababa wa aina hiyo, lakini pia kuondoa dhana hiyo potofu kuhusu maziwa ya mama hayana uhusiano wowote na kuongeza nguvu za kiume na kukata arosto ya pombe," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa jambo hilo halijitokezi tena ndani ya jamii kama wengi walivyokuwa wakiamini na sasa wameacha kutumia maziwa hayo na kuwapunja watoto.

Alionya jamii kuondokana na elimu isiyofaa ya mama kutumia maziwa na chakula mbadala na badala yake anyonyeshe mtoto wake maziwa kwa miezi sita bila chochote ili kumjenga mtoto mwenye afya njema kwaajili ya kujenga taifa imara.

Alisema jukumu la baba kwa mama anayenyonyesha ni kumwandalia mazingira ya kupata huduma stahiki wakati wa kuonyoshesha ili kumwondolea mawazo.

"Tunatambua jukumu la baba katika kumsaidia mama kunyonyesha vyema mtoto wake, katika kuadhimisha wiki hii, tunaendelea kuhimiza wazazi wote kushirikiana na mtoto apate virutubisho muhimu," alisema.

Alihimiza ruhusa za likizo kwa mama anayenyonyesha ya siku 84 kwa mtoto mmoja na siku 100 kwa watoto zaidi ya mmoja na siku tatu za baba kwaajili ya kumwangalia mtoto kwa wiki ya kwanza.

Alitaja hatua zinazichukuliwa na serikali katika kumwezesha mama kunyonyesha vizuri kuwa ni kutunga sheria ya ajira na uhusiano kazini, inayotambua unyonyeshaji ni haki ya mtoto na kutoa mafao ya mama anayenyonyesha.

Pia, alisema mwajiri haruhusiwi kumpangia mjamzito kazi ngumu za usiku au kumnyanyasa kwa namna yoyote.

"Mfumo huu haunufaishi wafanyakazi walio katika sekta binafsi, kilimo na biashara, hivyo ni jukumu la baba na familia kuangalia suala hili kwa makini ili wajawazito na wanaonyonyesha wapewe muda wa kumpumzika na huduma nyingine muhimu," alisema Dk. Leyna.

Ofisa Lishe Mtafiti wa TFNC, Fatuma Mwasora, alihimiza mlo kamili kwa wajawazito na wanaonyonyesha, matumizi ya dawa za Folic Acid za kuongeza damu kabla na baada ya kujifungua ili kumjenga mtoto aliyekamilika.

# Bosi benki, wanafamilia watatu wafa kwa ajali

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

NDUGU watatu familia moja na mwingine mmoja wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na Scania katika Kijiji cha Mapatano, Kata ya Mbwewe, Bagamoyo mkoani Pwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema ajali hiyo ilitokea jana majira ya saa saa 8:30 usiku na kuhusisha gari lenye namba za usajili T 104 CBU Toyota Prado likitokea Dar es Salaam kwenda Same, likiendeshwa na Mkurugenzi wa Benki ya ABSA, Nechi Msuya.

Kamanda Lutumo alisema gari hilo liligongana na lori lenye namba za usajili T 881 DWU likiwa na tela lenye namba za usajili T888 DWU likiendeshwa na Philipo Mtisi (43) likitokea Arusha kwenda Dar es Salaam.

Aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni dereva wa Toyota Prado, Nechi Msuya, Dayana Mageta, Wakili Dk. Nora Msuya ambaye alikuwa Mkufunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar Es Salam na abiria mwingine wa kike anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 30-35 jina halikufahamika.

Lutumo alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Toyota Prado kuhama kutoka upande wa kushoto kwenda kulia kisha kugongana uso kwa uso na lori hilo.

Alisema miili ya waliofariki dunia katika ajali hiyo imehifadhiwa katika Zahanati ya Lugoba ikisubiri uchunguzi wa daktari na kukabidhiwa kwa ndugu kwa mazishi.

Aidha, taarifa kutoka chanzo cha kuaminika zinaeleza kwenye familia ya Msuya wamezaliwa watoto wanne na kwamba watatu kati yao wakiwamo wa kike wawili na mmoja wa kiume wamefariki dunia huku mmoja ambaye anafanya kazi mkoani Dodoma akibaki peke yake.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani limetoa wito kwa madereva na watumiaji wa barabara kuchukua tahadhari na kuzingatia sheria za usalama kuepukana na ajali zinazoweza kusababishwa na uzembe.

Vilevile madereva wametakiwa kutotumia vileo wanapoendesha vyombo vya moto na kwamba tabia hiyo imekuwa chanzo cha kusababisha ajali za barabarani.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, aliandika: "Tumempoteza Dk. Norah Msuya, mkufunzi wa sheria za utawala katika Chuo Kikuu cha Mzumbe. "Ninamwomba Mungu aipe nguvu familia yake katika kipindi hiki kigumu. Nimejitahidi kuandika mistari michache lakini nimeshindwa. Mhadhiri bora na zaidi ya yote mwanadamu mwenye kipaji. Roho yake ipumzike kwa amani.

Mmoja wa marafiki wa Dk. Msuya, mwanahabari Idda Mushi, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Kifo ni mtihani sana, kifo ni fumbo, kwakweli Wakili Dk. Norah Msuya...Wana Kibosho Girls 1995 tumepigwa na kitu kizito. Siku imekuwa chungu baada ya ajali ya ndugu yetu, rafiki yetu kipenzi chetu kufariki dunia akienda msibani Same, mkoani Kilimanjaro."



# NHC yashauri 'uswahilini' kubomolewe

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limeishauri serikali kuifanya sekta ya nyumba kuwa kipaumbele cha taifa na kuja na mkakati wa kubomoa nyumba zilizojengwa bila mpangilio katika maeneo muhimu nchini na kujenga makazi mapya.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, alitoa ushauri huo jana alipojibu maswali wakati wa semina ya waharíri wa vyombo vya habari katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa sekta hiyo ikishakuwa kipaumbele cha taifa, kodi za bidhaa za ujenzi, pia zinazotozwa wakati wa ununuzi wa nyumba, zitaondolewa na hivyo wananchi kupata nyumba kwa gharama nafuu.

Alisema kuna haja kuyaangalia maeneo ambayo yana nyumba nyingi zilizojengwa bila ubora, akitolea mfano nyumba za Manzese, mkoani Dar es Salaam, ambazo zimejengwa pasi na kuzingatia mpangilio wa kisheria ili yaboreshwe kwa kujengwa nyumba za kisasa na wananchi waishi katika nyumba bora.

Mkurugenzi huyo pia alisema shirika linaendelea kuishawishi serikali kutoa rukhsa kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi kununua na kuwekeza ardhi ya Tanzania. Iondoe vikwazo vyote vinavyowazuia Watanzania wanaoishi ughaibuni pamoja na raia wa mataifa mengine kushiriki katika kuwekeza katika sekta ya uendelezaji miliki (Real Estate).

Alisema kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika nyumba za gharama nafuu tayari serikali imeshaanza jitihada kwa kuondoa kodi hiyo katika ununuzi wa nyumba zilizo chini ya Sh. milioni 50 kuanzia mwaka huu wa fedha.

Katika wasilisho lake kwa wahariri jana, Hamad alisema NHC inaishauri serikali kuanzisha mfuko wa maalum wa ruzuku ya nyumba za gharama nafuu.

Vilevile, aliishukuru serikali kwa kutoa kibali kwa NHC kukopa Sh. bilioni 173.9 kwa ajili ya kumalizia miradi ya Morocco Square na Kawe 711.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, NHC imeendelea kuongeza mapato yake hadi kufikia Sh. bilioni 257.47 mwaka 2022 kutoka Sh. bilioni 144.42 mwaka 2021.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2021/22, mapato ya kodi yamepanda hadi kufikia Sh. bilioni 90.76 kutoka Sh. bilioni 89.23 mwaka 2020/21.

"Mauzo ya nyumba yamepanda kutoka Sh. bilioni 29.33 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 121.95. Mapato ya miradi ya ukandarasi yamekua kutoka Sh. bilioni 25.6 mwaka 2020/21 hadi kufikia Sh. bilioni 43.98 mwaka 2021/22," alifafanua.

Hamad alibainisha kuwa thamani ya mali za shirika kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2022, zilikuwa Sh. trilioni 5.04.

Aliitaja miradi wanayotekeleza inajumuisha uboreshaji wa miji kwa kuvunja majengo ya zamani na kujenga mapya, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na uendelezaji wa vitovu vya miji.

Pia alisema ukamilishaji wa miradi iliyosimama tangu mwaka 2018 unaendelea, ukigusa mradi wa Morocco Square Sh. bilioni 137 ambao umekamilika kwa asilimia 97 na umeanza kupata wapangaji na wanunuzi wa nyumba; miradi ya Kawe 711 Sh. bilioni 105.1 na Golden Premium Sh. bilioni 71.1 mazungumzo kati yao na makandarasi yanaendelea.

Alibainisha kuwa hadi sasa wanadai jumla ya Sh. bilioni 23.808 toka kwa wateja wao, akionya kuwa wadaiwa hao wako mbioni kutangazwa katika vyombo vya habari na hawatokuwa na nafasi ya kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

Alisema wameweka utaratibu wapangaji wapya sasa lazima waweka amana ya ufunguo - kiwango ambacho ni sawa na malipo ya pango kwa miezi mitatu. Kwa waliokuwa wamepata nyumba zao pasi na kulipa kiwango hicho, wamepewa muda hadi Desemba mwaka huu kukilipa.

NHC ilianzishwa mwaka 1962 kwa Sheria Na. 45 kwa lengo la kuwapatia wananchi makazi bora.



Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), James Mlowe (kulia), akikabidhi taarifa za michango kwa Mwanachama wa Mfuko, huo aliyetembelea banda la PSSSF katika maonyesho ya kimataifa ya wakulima Nanenane, kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaleta mwekezaji mpya mazao kilimo

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema tatizo la wakulima wa matunda na mboga kuharibikiwa kwa mazao yao kutokana na kukosa soko, sasa litakwua historia.

Hiyo ni baada ya kumwalika mwekezaji kutoka Russia aliyeingia mkataba wa kujenga mitambo ya kukausha mazao nchini.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema hayo jana baada ya kutembelea Banda la Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), katika Maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi katika Viwanja vya John Mwakangale jijini hapa.

"Juzi nilikuwa nchini Urusi na nilikutana na mwekezaji mkubwa na nimemwalika nchini. Nilimwambia aje akutane na wewe Waziri wa Kilimo kwa ajili ya mazungumzo. Ana mitambo ya kukausha haya mazao yetu ambayo huwa yanaharibika kwa kuoza kama nyanya, zabibu, ndizi na mazao mengine. Nadhani akifanikiwa kuwekeza tutamaliza hilo tatizo la wakulima kuharibikiwa mazao yao wanapokosa soko," alisema.

Waziri Mkuu alisema Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, atakapokutana na mwekezaji huyo, watakubaliana zaidi jinsi ya kuongeza nguvu kwenye mitambo iliyopo kwa sasa ambayo haijitoshelezi. Alisema mitambo hiyo pia itasaidia kukausha maembe, machungwa na mengineyo ambayo yatauzwa kwa thamani kubwa kama mazao yasiyokaushwa.

Majaliwa alilazimika kueleza kuhusu mwekezaji huyo baada ya kuelezwa kuwa COSTECH imetoa Sh. milioni 400 kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Makutupora Dodoma kwa ajili ya kutengeneza mitambo ya kuongeza thamani kwenye zao la zabibu.

Ofisa Mwandamizi wa Uratibu wa Utafiti kutoka COSTECH, Dk. Deogracious Protas, alimweleza Waziri Mkuu Majaliwa kiasi hicho cha fedha kimetengeneza maabara ya kisasa ya kuwasaidia wakulima.

Alisema hivi sasa wakulima wanapozalisha zabibu hupelekwa TARI Makutupora wanafundishwa kuziongezea thamani na hivyo kuuzwa kwa bei rafiki ya mkulima tofauti na awali walikuwa wakiuza kwa bei ya chini.

Mtafiti kutoka TARI Makutupora, Phelister Mpole, alimweleza Waziri Mkuu kuwa hukausha zabibu kwa kutumia kaushio maalum ambalo lina karatasi ya kufyonza mwanga wa jua, ili kupunguza siku za kukaushia.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema TARI Makutupora wanatoa mafunzo kwa wakulima wadogo juu ya ukaushaji wa zabibu.

"Pale Chinangali tunajenga kiwanda kikubwa ambacho kitakuwa kina mitambo kuanzia ya kukaushia mpaka ya kutengeneza mvinyo. Wakulima watakapovuna zabibu zao badala ya kuuza zabibu matunda pia wataweza sasa kuchagua kutengeneza juisi au kukausha ili iwe na thamani zaidi," alisema.

## Watumishi sita wadaiwa kufunga ndoa feki ili kuingiza ndugu NHIF

**Na Moses Ng'wat,** ILEJE

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Songwe umewashtaki kwa wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, watumishi sita waliobainika kughushi vyeti vya ndoa kwa kupeleka wenzi feki ili kupata huduma za matibabu.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Songwe, Simon Mmbaga, alibainisha hayo jana wakati akiwasilisha taarifa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kuhusu mfuko huo na kuwaomba madiwani kusaidia kuelimisha jamii kuhusu kujiunga na mfuko.

Mmbaga alisema baada ya NHIF kufanya ukaguzi kwa kupitia mifumo ya mfuko huo katika mkoa wa Songwe, ilibaini watumishi sita waliwachukua kaka na dada zao na kuwapeleka ofisi za wakuu wa wilaya kwa kuwatambulisha kuwa ni wenza wao, ili waweze kupatiwa vyeti vya ndoa.

Alisema watumishi hao waliamua kufanya udanganyifu huo ili kuwezesha ndugu zao hao kukidhi vigezo na masharti ya mfuko ikiwemo kuwasilisha vyeti vya ndoa na nyaraka zingine za kiutumishi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Nuru Kindamba, alikiri watumishi wake wawili kubainika kufanya udanganyifu kwenye mfuko huo kwa kuwaingiza ndugu zao ambao hawatambuliwi kisheria na mfuko huo.

Kindamba alisema ni kweli suala hilo liko ofisini kwake na tayari taratibu za kiutumishi zimeanza kuchukuliwa, ikiwamo watumishi hao kuamriwa kurejesha fedha.

# MOI yaja na mkono bandia wa umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imeanzisha huduma mpya ya utengenezaji wa mkono wa umeme ambao una uwezo wa kufanya kazi mbalimbali kwa asilimia 60 hadi 70 na tayari watu watano wamehudumiwa.

Gharama zake nchini ni Sh. milioni 15 wakati nje ya nchi ni Sh.milioni 30 hadi 60.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya MOI kwa kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na mipango ya mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema mkono huo umetengenezwa ili kumsaidia mtu kula na baadhi ya vitendo vilivyopangiliwa kwenye mfumo wa umeme.

"Wananchi tuliowawekea imesaidia kufanya baadhi ya kazi ambazo walitegemea kwa asilimia 100 wasingeweza kuzifanya, lakini unafanya kazi kwa asilimia 60 hadi 70 ya kazi," alisema.

"Huduma hii ni mpya tulipeleka wataalam wetu kwenda kusoma Ujerumani na tayari wananchi wachache wamenufaika, tumejipanga kuitoa huduma hii kwa wananchi wenye uhitaji huo," alisema.

Aidha, alisema suala la gharama za matibabu ya mifupa litakwenda kupungua zaidi kwa kufanya ununuzi wa vifaa kutoka moja kwa moja kwenye viwanda kwa kushirikiana na MSD.

"Tayari huu mpango tumeanza kushirikiana na MSD ili kupunguza gharama kwa mfano kifaa kinauzwa Shilingi milioni mbili, kule tunapata kwa Shilingi milioni moja pungufu ya gharama hatua hii itapunguza gharama kutoka asilimia 20 hadi 40," alisema.

Akizungumzia kuhusu wagonjwa wasio na uwezo, alisema serikali kupitia taasisi hiyo ilitoa misamaha ya Sh. bilioni 6.5 ndani ya miaka miwili kwa wananchi wasio na uwezo na ambao pia hawakuwa na bima za afya ili kuwawezesha kupata huduma za uchunguzi, dawa na upasuaji.

Kuhusu upasuaji wa kibingwa bobezi, alisema wagonjwa 14,574 ndani ya miaka miwili walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na 13,618 wa miaka miwili iliyopita (2019/20 mpaka 2020/21) ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.4.

Alisema gharama za matibabu hayo ndani ya nchi zilikuwa Sh. bilioni 36.4 na kama wangepelekwa nje ya nchi kwa matibabu Sh. bilioni 231.6 zingetumika, serikali imeokoa Sh. bilioni 195.2.

Alisema huduma ya kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua wamefanyiwa wagonjwa 31 na gharama za upasuaji huo hapa nchini ni kati ya Shilingi milioni nane hadi 16 na nje ya nchi ni zaidi ya Sh. milioni 40.


# JOB ADVERTISEMENT

**Mlimani SACCOS Ltd (MSL) is a Saving and Credit Cooperative Society registered in year 2003 with the aim of serving the university of Dar es Salaam employees, their immediate families and retiree with financial Services at affordable costs using the Cooperative Business Model. MSL is currently is looking to hire qualified and eligible Tanzanians to fill vacant positions as part of its effort to build a strong, innovative and efficient Management team that will fast track the realization of its mission.**

**1.0 TITLE: MANAGER/CHIEF ACCOUNTANT 1 POSITION**

**1.1 Position Description**

The Employee shall serve the 'Employer' in the Capacity of **MLIMANI SACCOS MANAGER/CHIEF ACCOUNTANT** and in that capacity He /She shall be responsible to the MSL Board for planning, co-ordination, and guiding the SACCOs Management in implementing the SACCOS's Strategic Objectives and Policies.

**1.2 Duties and Responsibilities. Provided in MSL Job Description Manual**

**1.3 Professional and Academic Requirements**

- Bachelor of Commerce (Finance/Banking/Accounting) OR Bachelor of Business Administration OR B.A Economics, or any other Degree coupled qualifications in Finance and accounting OR any equivalent qualifications from accredited University/Institution
- CPA(T)
- Age between 25 – 55 years.
- At least three years' relevant experience at a management level in a SACCOS or Financial institution. (Micro-Finance).
- Certificate of good conduct.
- Possession of MBA, Certifications in SACCOS's operations, first degree in Cooperative Management, Business Management, Microfinance, Marketing, Entrepreneurship will be an added advantage.

**1.4 Other Requirements**

- Experience in strategic management including planning, goal setting, implementation, monitoring and evaluation and reporting, strong team building skills and able to manage, guide and lead employees to ensure maximum efficiency from the human resource.
- Working knowledge of all statutory legislation and regulations
- Computer literacy and skills (Advanced user of MS Word, Excel), knowledge and proficiency in computerized accounting operations, knowledge of computerized financial management system
- In-depth understanding of Generally Accepted Accounting Principles (GAAP)

**2.0 TITLE: ASSISTANT ACCOUNTANT 1 POSITION**

**2.1 Position Description**

The Assistant Accountant shall report directly to the Manager/Chief Accountant of MSL and shall help MSL to make critical financial decisions by collecting, tracking, correcting and communicating the financial position of MSL finances. He/she shall be responsible for recording transactions, compiling and analyzing data, perform financial audits, reconciling bank statements assist with budgets and financial forecasting, compute taxes, and report His or Her findings to MSL Manager/Chief Accountant for onward presentation to the Board. He or She shall ensure that financial records of MSL are accurate throughout the year.

**2.2 Duties and Responsibilities. Provided in MSL Job Description Manual**

**2.3 Professional and Academic Requirements**

- Bachelor of Commerce (Finance / Accounting) OR equivalent qualifications from accredited University/Institution
- Age between 20 – 55 years.
- At least One years' relevant experience at a management level in a SACCOS or Financial institution. (Micro-Finance).
- Experience with accounting software is a plus
- Certificate of good conduct.
- Possession of MBA, Qualifications in SACCOS's operations, First degree in Cooperative Management, Business Management, Microfinance, Marketing, Entrepreneurship will be an added advantage. Hands on experience with accounting software is also a plus.

**3.0 TITLE: LOAN OFFICER 1 POSITION**

**3.1 Position Description**

The Loan Officer shall report directly to the Manager/Chief Accountant of MSL and shall be responsible for reviewing, authorizing and recommending loans for approval. He or She shall meet with applicants to determine their creditworthiness before deciding whether or not they will offer them an emergence loan or a long term loan. He or She shall go through each application individually, looking at what type/amounts an individual can afford based on specific principles. The Loan Officer shall at any given time, stay current with lending regulations, the economy and market rates.

**3.2 Duties and Responsibilities. Provided in MSL Job Description Manual**

**3.3 Professional and Academic Requirements**

- Bachelor of Commerce (Finance /Accounting) OR equivalent qualifications from accredited University/Institution
- Age between 20 – 55 years.
- At least One years' relevant experience at a management level in a SACCOS or Financial institution. (Micro-Finance).
- Experience with accounting software is a plus
- Possession of MBA, Qualifications in SACCOS's operations, First degree in Cooperative Management, Business Management, Microfinance, Marketing, Entrepreneurship will be an added advantage.
- Customer service-oriented with exceptional marketing skills.

**4.0 RENUMERATIONS**

Competitive salaries and benefits will be offered for each of the positions

**5.0 MODE OF APPLICATIONS**

Interested applicants should submit their applications attached with CVs and certified copies of their Certificates to:

Mlimani SACCOS Ltd,
University of Dar es Salaam PO Box 35091 Dar es Salaam
Or send soft copies of their applications with all relevant attachments to:
Email: mlimanisaccoslimited@gmail.com
The deadline for receiving applications is 11:59 PM on the 20th day of August 2023

**6.0 ADDITIONAL INFORMATION**

a. Only those applications that meet minimum qualifications will be considered.
b. Shortlisted candidates will be informed and shall be required to attend interviews any time between 21 August 2023 and 26 August 2023
c. The MSLs' Board recruitment decision is final
d. Visit SCCULT Website at https://sccult.tz for additional information on this Job Advertisement

217536102

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## NHC iungwe mkono kukuza sekta ya nyumba nchini

**KATIKA** vipaumbele ambavyo Shirika la Nyumba Nchini (NHC) ilivyojiwekea ni kuendelea kuishawishi serikali kuwa nyumba ni kipaumbele cha Taifa.

Nchi yoyote duniani ambayo imewekeza katika nyumba, wananchi wake wanakuwa na uhakika wa kuishi mahali bora, salama na penye amani.

NHC ambayo ilianzishwa mwaka 1962 ikiwa ni mwaka mmoja tu baada ya kupata uhuru wa Tanganyika ilikuwa na dhamira ya kuwapatia Watanzania makazi bora.

Nyumba zilizojengwa kwa matope na kuezekwa kwa makuti zilibomolewa na wananchi wakajengewa nyumba bora za matofali na bati.

Ndiyo maana katika mikoa mbalimbali nchini kumejengwa nyumba za shirika hilo ambazo wananchi walipewa kwa mkopo na walipomaliza wakakabidhiwa kuzimiliki.

Nyumba hizo zilijengwa kwa mtindo wa kuishi kijumiya ambazo upande mmoja ulikuwa maalumu kwa mmiliki na upande mwingine kwa ajili ya wapangaji ili kodi inayopatikana mwenye nyumba aweze kulipa mkopo wa NHC.

Kwa mfano katika Jiji la Dar es Salaam, nyumba za NHC zilijengwa maeneo ya Magomeni, Kinondoni, Mwananyamala, Keko na maeneo mengine.

Katika eneo la Magomeni ambako ni maarufu kama Magomeni Mapipa, wakazi wa eneo hilo miaka ya nyuma walijengewa nyumba kwa kuezeka kwa mapipa. Pipa linachanwa katikati na kuezekwa na eneo hilo kupata umaarufu wa jina hilo.

Shirika la Nyumba lilipoanzishwa likaona umuhimu wa kuwajengea wananchi nyumba bora ambazo watazilipa kwa mkopo na mpaka sasa baadhi ya wakazi wa eneo hilo wanaendelea kuishi kwenye nyumba zilizojengwa kipindi hicho na wengine waliofanikiwa walizinunua na kuzibadilisha.

Katika nchi za Afrika Mashariki kama Rwanda na Kenya, zimepiga hatua katika kuwajengea wananchi wake nyumba bora baada ya kuingia ubia na wawekezaji.

Faida ya kuingia ubia katika nyumba ni kwamba mwekezaji anapomaliza muda wake nyumba inabaki nchini kwa sababu haondoki nayo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, akieleza mikakati ya shirika hilo kwa wahariri na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, amesema wanaangalia maeneo ambayo yana nyumba nyingi zilizojengwa bila ubora, kama Manzese ili yaboreshwe kwa kujengwa nyumba za kisasa na wananchi waweze kuishi kwenye nyumba bora.

Shirika hilo linafanya juhudi kuwaruhusu Watanzania wanaoishi nje ya nchi kununua na kuwekeza ardhi ya Tanzania, na linaendelea kuishawishi serikali kuondoa vikwazo vyote vinavyowazuia Watanzania wanaoishi ughaibuni pamoja na raia wa mataifa mengine kushiriki katika kuwekeza kwenye sekta ya uendelezaji miliki (Real Estate).


Kwa sasa Shirika hilo linaendeleza na kukamilisha miradi ya nyumba zake ambazo zilikuwa hazijakamilika kwa muda mrefu tangu mwaka 2018, ukiwamo mradi wa Morocco Square, uliogharimu Sh. bilioni 137 na kukamilika kwa asilimia 97 na tayari umeanza kupata wapangaji na wanunuzi wa nyumba.

Mradi wa Morocco Square umejengwa kwa ajili ya nyumba za kuishi, maduka makubwa ya kisasa, sehemu za starehe, hata mtu anayeishi kwenye nyumba hizo hata kuwa na sababu ya kutoka kwenda kutafuta huduma hizo nje ya jengo.

Kadhalika mradi wa Kawe maarufu 711, uliogharimu Sh. bilioni 105.1 na mradi wa nyumba za kuishi wa Golden Premium uliogharimu Sh. bilioni 71.1, mazungumzo kati ya shirika na wakandarasi ili kuendelea na kazi yanaendelea.

Kwa mikakati hii ya NHC tunaona Tanzania kutoka kivingine kwa upande wa majengo kama tunavyoshuhudia katika baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam na Makao Makuu ya Nchi, Dodoma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Vijana waonyeshwe fursa zilizoko vijijini

**VIJANA** kuhamia mijini na kuvikimbia vijiji ni wimbi linaloikumba kila kona ya nchi hii kuanzia Mtwara hadi Mpwapwa.

Imani yao ni kutafuta ajira au kufanya biashara kwa urahisi ili kujikimu hivyo kuona bora kuishi kwenye majiji kama Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam. Ipo pia sababu nyingine ya kukimbilia mijini ambayo imekuwa ikizungumzwa zaidi na baadhi ya vijana hao ambayo ni ugumu wa maisha vijijini.

Wanajitetea kwamba hali ya maisha huko ni ngumu na inachangiwa na ukosefu wa miundombinu ya kuwezesha kumudu maisha.

Kutokana na mtindo huo, baadhi yao wanakimbilia kwenye biashara ndogondogo kama kuuza pipi, biskuti, pweza na matunda ambayo ni vigumu kuwa kwamua kiuchumi. Wakati hao wakiwa katika mazingira hayo, wengine hujiingiza katika makundi ya kihalifu, ambayo yanaweza kuhatarisha maisha yao bila wao kujua au wakiwa wanajua.

Hivyo, ili waweze kuinuka kiuchumi, wanashauriwa kubadili fikira na mitazamo na mtindo wa kukimbilia mijini, badala yake watumie fursa za kiuchumi zilizopo vijijini zikiwamo za kilimo, ufugaji, uvuvi, sanaa, shughuli za kitamaduni na ubunifu ili waweze kujiletea maendeleo.

Inaelezwa kuwa vijijini kuna biashara nyingi ikiwamo kuuza mazao ya vyakula yatokanayo na kilimo, uvuvi au ufugaji. Kijana anaweza kununua mazao wakati wa msimu wa mavuno na kuhifadhi. Kupitia mtindo huo, wakati wa uhaba wa chakula kijana anaweza kuuza kwa bei nzuri, lakini pia anaweza kufungua duka akawa anakwenda mjini kununua bidhaa na kuiuza kwa bei ya rejareja au jumla.

Hayo ni kwa mujibu wa mfanyabiashara, Thomas Ngawaiya ambaye anasema kuwa kwa sasa karibu vijiji vyote nchini vina huduma ya umeme, ambayo inaweza kutumika kubuni biashara mbalimbali ikamwezesha kijana kuendesha maisha yake kwa mafanikio.

> **Binafsi ninaunga mkono njia hiyo ya kuwainua vijana kupitia fursa zilizopo vijijini, kwani zinaweza kuwasaidia kuepuka kukosa shughuli za kufanya na kutojiingiza katika makundi hatarishi.**

Ngawaiya, ambaye anasema kuwa pamoja na biashara mbalimbali anayofanya pia ni mkulima wa mihogo na korosho Handeni mkoani Tanga, anaamini kuwa hiyo ndiyo njia ya vijana kiunuka kiuchumi. Katika ufafanuzi wake, anasema kwa sasa kuna soko la mhogo China, na kwamba serikali imekuwa ikihimiza vijana kujikita kwenye kilimo cha mazao mbalimbali ya biashara na matunda ili wajipatie maendeleo.

Binafsi ninaunga mkono njia hiyo ya kuwainua vijana kupitia fursa zilizopo vijijini, kwani zinaweza kuwasaidia kuepuka kukosa shughuli za kufanya na kutojiingiza katika makundi hatarishi.

Ni wazi kwamba, wanapojiingiza katika makundi hayo, ni wazi hata usalama wao unakuwa mashakani. Hivyo, ninadhani ni vyema kuunga mkono ushauri huo wa kubaki vijijini na kutumia fursa zilizopo huko. Binadamu aliyekamilika ana fikra za namna gani ajikwamue, atengeneza fedha, ili maisha yake yawe mazuri, hakuna anayependa kuishi maisha ya mateso, hivyo ni vyema vijana wachangamkie fursa za vijijini.

Hilo linaweza kufanyika iwapo vijana wenyewe watajiuliza swali hili kuwa, hivi ni kweli fursa za kiuchumi ziko mijini tu? Jibu ni kwamba si kweli, bali iwe mijini au vijijini, fursa hizo zipo kote.

Ikumbukwe, hata mijini kuna changamoto zake kama ambavyo nimeeleza awali, lakini pia bila kusahau kuwa wapo waliokimbilia mijini na kuishia kula mlo mmoja kwa siku, kutokana na ugumu wa maisha, wengine kulala mitaroni na vituo vya mabasi.

Hivyo ni wazi maeneo yote yana changamoto zake, ila jambo la msingi ni kutafakari kwamba kabla ya kuchukua hatua za kukimbilia huko, kwani inaweza kuwa ni sawa na kuruka majivu na kukanyaga moto.

Kimsingi, kijana mwenye nguvu za kuzalisha mali kuishi mjini bila kuwa na kitu cha maana kinachomwingizia fedha, siyo ujanja, hivyo ni vyema utazame kwa upana fursa zinazoweza kupatikana vijijini.

# Serikali yasikia kilio wafanyakazi wa TPL

**Na Munir Shemweta,** ARUMEERU

SERIKALI imesikiliza kilio cha waliokuwa wafanyakazi katika shamba la Tanzania Plantation lililoko wilaya za Arusha na Arumeru, kwa kuwapatia maeneo kwa ajili ya kujenga makazi na shughuli za kilimo na ufugaji.

Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kusikia kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi hao, ameridhia wananchi 102 wapewe kipaumbele cha kwanza katika kupewa ardhi, amesema Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula.

Akizungumza na wananchi wa kitongoji cha Lucy eneo la Bwawani wilayani Arumeru juzi, Dk.Mabula alisema kutokana na uamunifu waliokuwa nao wananchi hao kwa muda mrefu katika eneo hilo kwa kuendelea kutunza mashamba hata pale wawekezaji walipotetereka, serikali itawapatia maeneo ya kujenga nyumba za makazi na kumilikishwa kisheria.

Waziri aliongeza kuwa kama hiyo haitoshi, Rais Samia kwa kutambua kuwa wananchi hao bado ni wakulima na wana nguvu za kufanya shughuli za uzalishaji, ameelekeza pamoja na kupatiwa eneo la ujenzi wa nyumba, wapatiwe pia walau ekari mbili mbili kwa ajili ya kilimo.

Dk. Mabula alibainisha kuwa katika eneo hilo la shamba la Tanzania Plantation Ltd, kuna wananchi 486 waliovamia mashamba na kuweka bayana kuwa pamoja na ukiukwaji wa taratibu walioufanya, Rais ameelekeza wazingatiwe katika kupatiwa maeneo kwa kufuata taratibu.

"Pia wapo wasamaria wema 27 waliojitolea maeneo yao kwa serikali ili kujengwa shule na zahanati. nao imeelekezwa kuingizwa katika utaratibu wa kupatiwa maeneo," alisema.

Dkt Mabula pia alisema kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi wa wananchi hao, serikali imeamua kuwapatia maeneo ya makazi kwa gharama ya Sh. 601 kwa mita moja ya mraba huku mashamba yakitolewa kwa Sh. milioni 2.5 kwa ekari moja.

Serikali ilikabidhiwa mashamba yaliyokuwa yakimilikiwa na Tanzania Plantations Ltd baada ya kukamilisha taratibu za kuyatwaa.

Makabidhiano ya mashamba hayo yaliyokuwa yakijulikana kama Karangai na Lucy Estates yalihitimisha mgogoro uliodumu kwa muda mrefu baina ya serikali na kampuni hiyo sambamba na ule wa wananchi na kampuni hiyo kutokana na wananchi kuuziwa baadhi ya maeneo katika mashamba yaliyobatilishwa.

Mgogoro kati ya Tanzania Plantations Ltd na serikali uliibuka mwaka 1999 baada ya kampuni hiyo kupinga ubatilisho wa mashamba uliofanywa na serikali kwa kushindwa kutimiza masharti ya umiliki jambo lililoifanya kampuni hiyo kufungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mwaka 2015.

Hata hivyo, katika kutafuta suluhu nje ya mahakama, serikali kupitia Wakili Mkuu wa Serikali, Mei 15, 2019 iliwasilisha ombi la majadiliano na mdai na mahakama iliridhia pande mbili kumaliza suala hilo nje ya mahakama ndipo serikali ilikubali kulipa Sh. bilioni 5.7 kwa ajili ya fidia ya mashamba.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula akiangalia mashine ya kuchakata mkonge alipotembelea eneo la shamba la Tanzania Plantation, wilayani Arumeru mkoa wa Arusha juzi. **PICHA: WANMM**




TANGAZO

# TOL Gases Limited

We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## EXTRACT OF THE STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

| | 2022<br>TZS '000 | 2021<br>TZS '000 |
|---|---|---|
| Revenue | 25,558,350 | 24,849,905 |
| Cost of sales | (13,746,778) | (14,532,314) |
| **Gross profit** | **11,811,572** | **10,317,591** |
| Other income | 161,109 | 28,999 |
| Operating expenses | (4,631,715) | (4,877,395) |
| Trade receivables impairment release | (9,544) | - |
| **Operating profit** | **7,331,422** | **5,469,195** |
| Finance costs | (1,134,852) | (991,084) |
| **Profit before tax** | **6,196,570** | **4,478,111** |
| Income tax expense | (2,716,334) | (1,183,480) |
| **Profit for the year** | **3,480,236** | **3,294,631** |
| Other comprehensive income | - | - |
| **Total comprehensive income** | **3,480,236** | **3,294,631** |
| Earnings per shares (TZS) | | |
| – Basic | 60.52 | 57.29 |
| – Diluted | 60.52 | 57.29 |

## EXTRACT OF STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2022

| | 2022<br>TZS '000 | 2021<br>TZS '000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current Assets** | | |
| Property, plant and equipment | 36,086,300 | 26,927,827 |
| Right-of-use assets | 328,068 | 335,125 |
| Intangible asset | 225,258 | 296,478 |
| Advances to suppliers | - | 446,856 |
| | **36,639,626** | **28,006,286** |
| Current assets | | |
| Inventories | 2,337,579 | 4,089,520 |
| Trade and other receivables | 6,879,076 | 5,019,850 |
| Cash and bank balances | 5,098,300 | 4,312,902 |
| Asset held for sale | 2,674,275 | 2,674,275 |
| Advances to suppliers | 2,370,249 | 923,077 |
| | **19,359,479** | **17,019,624** |
| **TOTAL ASSETS** | **55,999,105** | **45,025,910** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Share capital | 5,750,596 | 5,750,596 |
| Share premium | 6,762,049 | 6,762,049 |
| Retained Earnings | 12,937,553 | 11,757,384 |
| | **25,450,198** | **24,270,029** |
| **Non-current liabilities** | | |
| Long term borrowings | 8,813,437 | 11,927,120 |
| Lease liabilities | 59,627 | 59,817 |
| Deferred tax liability | 3,878,562 | 3,387,620 |
| | 12,751,626 | 15,374,557 |
| **Current liabilities** | | |
| Trade and other payables | 3,721,310 | 2,115,619 |
| Lease liabilities | 11,386 | 11,385 |
| Tax payable | 1,004,532 | 208,976 |
| Bank overdraft | 7,350,103 | - |
| Cylinder deposits | 517,137 | 497,464 |
| Current portion of loans | 5,192,813 | 2,547,880 |
| | **17,797,281** | **5,381,324** |
| Total liabilities | **30,548,907** | **20,755,881** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **55,999,105** | **45,025,910** |

217537002



# Wanaharakati walaani mauaji ya kinyama

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WANAHARAKATI 20 wanawake wanaopinga vitendo vya ukatili dhidi ya makundi maalumu katika Wilaya ya Moshi, Kilimanjaro, wamelaani mauaji ya kikatili ya Mary Mushi (30), anayedaiwa kuuawa madai ya wivu wa mapenzi

Pia wamelaani tukio la ubakaji lililofanywa dhidi ya mwanafunzi wa darasa la pili katika kijiji cha Boro kilichoko eneo la Kibosho.

Jana, wanaharakati hao wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Jenifa Kassim, walitoa tamko hilo la kukemea vitendo hivyo, walipokutana katika mafunzo ya siku moja ya wahudumu ngazi ya jamii kutoka katika kata tano za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Mafunzo hayo yametolewa na Shirika la Kiraia la KWIECO, kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), yakihusu zaidi mbinu na harakati za mageuzi ya kijinsia ili kukomesha vitendo vya kutokuwa na usawa na unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo yao.

"Hatukubaliani na yanayoendelea Kibosho, watu wanauana kinyama. Ubakaji dhidi ya watoto huko Kibosho hauvumiliki na haukubaliki. Sisi kama Wanaharakati wanawake tunakemea na kulaani ukatili huu na tunaomba vyombo vya dola, hasa Polisi waingie kazini kuwasaka watu waliotekeleza ukatili kule Kijiji cha Boro na Kirima Juu-Usagara," alisema Kassim.

Mratibu wa mafunzo hayo yanayotolewa kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, Veronica Ullomi, alisema Kata zinaguswa na mradi huo ni Mwika Kusini, Mwika Kaskazini, Kibosho Magharibi, Oldmoshi Magharibi na Kiruavunjo Kusini.

Wadau wengine walioshiriki mafunzo hayo ni kutoka Ofisi ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Moshi, ambao waliahidi kutoa ushirikiano kwa wanaharakati wanawake ili kuhakikisha jamii inapata elimu na inashiriki katika harakati za kutokomeza vitendo vya ukatili.

Mary Mushi (30) mkazi wa Kibosho Kirima, aliuawa kwa kukatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake, kwa kile kilichodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi, Julai 31, mwaka huu.

Inadaiwa kuwa watu waliofanya unyama huo walimpigia simu saa 3:00 usiku kisha kuondoka naye na ambapo baada ya mauaji hayo, waliutupa mwili wake shambani kwao.

## Chuo cha ufundi chabuni pikipiki ya umeme jua

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHUO Cha Ufundi Arusha (ATC), kimekuwa cha kwanza nchini na Afrika, kubuni pikipiki inayotumia nishati ya umeme wa jua na inayodumu kwa miaka 17 na zaidi.

Akizungumza jana wakati akifungua kongamano la kimataifa la siku nne linalofanyika chuoni hapo, Kamishna wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lybwene Mtahabwa, alikipongeza chuo hicho, kuwa na teknolojia nyingi ambazo ni mkombozi kuelekea uchumi wa viwanda.

"Hapa nimejifunza mambo mengi yanayoendelea hasa teknolojia ya utengenezaji pikipiki isiyo na sauti pasipo kutumia mafuta ambayo kwa sasa yana gharama kubwa. Mtu akiwa nayo anachaji tu kwa dakika 20 anakwenda kilomita 200 kwa siku. Huu ni ubunifu mzuri na wa kwanza katika nchi zetu za Afrika Mashariki na kote kwa ujumla," alisema.

Pia alisema pikipiki hiyo itakuwa mkombozi hasa kwa vijana kwa kuwa wanaziendesha na kuzitumia katika biashara zao za usafirishaji wa abiria na mizigo, bila kutumia gharama kubwa.

Alisema ATC imebuni teknolojia ya kutumia maji ya ardhini na juu ya ardhi, kwa ajili ya kumwagilia mashamba na bustani kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mazao yenye tija na kuondokana na utegemezi wa mvua ambazo zimekuwa za mashaka kwa sasa.

"Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kutokuwa na mvua za uhakika na kwa teknolojia hii itatuwezesha nchi yetu kuwa na kilimo cha uhakika na kuleta chachu kwa viwanda na maendeleo zaidi," alisema.

Hata hivyo, alisema kupitia ubunifu na ugunduzi wa chuo hicho kuna teknolojia nzuri na rahisi za kuwawezesha wakulima nchini kujikomboa na kuondokana na utegemezi wa neema ya mvua.

"Lakini nashauri tuanze kujenga shauku kwa watoto wetu wenye umri wa miaka nane, waanze kujifunza masomo kuhusu teknolojia mbalimbali tutaona matokeo mazuri kwa kuwa hata ukitaka kufundisha uchawi au utaalamu wowote umri huu ndio mzuri," alisema.

Mkuu wa Chuo cha ATC,Dk. Musa Chacha, alisema chuo hicho, kimefanikiwa kubuni teknolojia hizo,kutokana na ushirikiano wa chuo hicho na vyuo viwili vya nchini Korea Kusini ambavyo ni Hanyang' na Seoul.

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# NOTICE

## 28TH ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the 28th Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 25thAugust, 2023 at 9.00a.m to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2021 Annual General Meeting held on 19th August, 2022.
3. Matters arising from minutes of the year 2021 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December, 31, 2022.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2023.
9. Election of Directors.
10. To set the place, date and venue of the next meeting.
11. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

member entitled to attend and vote at the Meeting is also entitled to appoint a proxy (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his/her stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz/nlulu@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).



# Simbachawene ahimiza uwajibikaji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi, Ofis ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amehimiza waajiri wote nchini kuwajibika katika kuwawajengea uwezo maofisa utumishi ili watekeleze majukumu yao ipasavyo.

Simbachawene alitoa kauli hiyo jana mkoani hapa alipokutana na kufanya mazungumzo na watumishi kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza katika ziara yake ya kikazi ya siku mbili.

Alisema katika kuboresha utumishi na rasilimali watu, idara hiyo ina jukumu la ufuatiliaji wa nidhamu, kupandishwa vyeo na uhuishaji wa taarifa za kiutumishi kwenye mfumo na kwa pamoja zinahitaji umakini, uwajibikaji na weledi.

Pia aliwaagiza maofisa utumishi kujaza taarifa za watumishi kwenye mfumo wa utumishi ili kurahisisha utendaji kama upandishaji wa madaraja na uwajibishaji wa masuala mbalimbali ya kinidhamu.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alisema serikali kupitia utendaji wa Ofisi ya Rais (Utumishi) imeendelea kuonyesha dhamira ya kuboresha utumishi wa umma na utawala bora nchini na kuahidi kuendeleza ushirikino katika kipindi chote cha ziara yake ya kikazi mkoani hapa.

"Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa kutupa upendeleo maana mkoa wa Mwanza umekuwa wa kwanza kufanya ziara ya kiutumishi na ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na wizara yako maana yake sasa upo 'site', alisema.

Waziri Simbachawene yuko mkoani Mwanza kwa ziara ya kikazi na pamoja na mambo mengine, anatarajiwa kukagua miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Wilaya za Kwimba na Misungwi.

TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### UTARATIBU WA ULIPAJI WA KODI YA ZUIO YA ASILIMIA MBILI (2%) KWENYE MALIPO YA UNUNUZI WA MADINI

Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 imefanya marekebisho ya kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332, Toleo la Mwaka, 2019 kwa kuanzisha wajibu wa kuzuia kodi ya mapato ya **asilimia mbili (2%)** kwenye malipo yanayohusika na ununuzi wa madini ya metali yenye thamani, madini ya vito na mawe ya vito (precious metals, gemstones and other precious stones), pindi yatakapouzwa na mchimbaji mdogo mwenye leseni na asiye na leseni. Utekelezaji wa mabadiliko haya ya sheria umeanza tangu tarehe **1 Julai, 2023.**

Kulingana na marekebisho yaliyofanyika kwenye sheria tajwa, mlipaji wa kodi ni Mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni. Ili kuwasilisha kodi hiyo TRA, Mfanyabiashara mdogo wa biashara ya madini (Broker) atazuia kodi wakati anafanya malipo kwenda kwa Mchimbaji kutokana na ununuzi wa madini ambao ataufanya kwenye vituo vya ununuzi wa madini (buying centers). Aidha, mfanyabiashara huyo mdogo (Broker) atakapouza madini yake kwenda kwa mfanyabiashara mkubwa (Dealer), hatakatwa kodi ya zuio.

Vilevile, pale ambapo Mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni atakapouza madini yake kwenda kwa Mfanyabiashara mkubwa wa biashara ya madini (Dealer), mfanyabiashara huyo atazuia kodi wakati wa kufanya malipo kwa mchimbaji kwenye Soko la Madini (Mineral markets) na kuiwasilisha kodi hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Ifahamike ya kwamba kodi itakayozuiwa na Mfanyabiashara wa biashara ya madini itakuwa ni kodi ya mwisho kwa mchimbaji wa madini kama ilivyobainishwa kwenye Kifungu cha 86(1)(g) cha Sheria ya Kodi ya Mapato. Hii inamaanisha kwamba, mchimbaji mdogo mwenye leseni au asiye na leseni hatawajibika tena kukadiriwa au kujikadiria kodi kwenye mapato ambayo **chanzo chake ni uuzaji wa madini tajwa hapo juu**.

Tunapenda kuwajulisha kwamba Maafisa wa TRA watakuwepo kwenye Masoko ya Uuzaji wa Madini ili kutoa huduma zitakazowezesha ulipaji wa kodi hiyo pamoja na kutoa ufafanuzi wa masuala ya kodi utakaohitajika.

Wafanyabiashara wadogo wa biashara ya Madini (Brokers) wanasisitizwa kuwa, pindi wanapofika kwenye masoko ya madini wahakikishe wanakuja na majina na Namba za Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) ya Wachimbaji wadogo wa madini ambao wamewakata kodi, ili kuwezesha kodi itakayokatwa iweze kuakisi kwenye TIN ya Mchimbaji husika badala ya Mfanyabishara wa madini (Broker/Dealer).

Wachimbaji wadogo ambao hawana TIN, huduma hiyo itatolewa kupitia Vituo na Masoko ya madini pamoja na Ofisi za Kodi za Mkoa. Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali tembelea Ofisi ya TRA iliyo karibu nawe au tumia anwani zifuatazo kuwasiliana nasi :-

Tovuti : **www.tra.go.tz**
Namba za Bure za Kupiga : **0800 750 075** au **0800 780 078** au **0800 110016**
WhatsApp : **0744 23 33 33**
Barua Pepe : **huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

Kidatah

A.J. Kidata
**Kamishna Mkuu**

217536302

# Jela miaka 30 unyang'anyi kutumia silaha

**Na Mwita Nyamhanga**

MKAZI wa Kijiji cha Soronet, Tarime mkoani Mara, Mwita Nyamhanga, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kukutwa na hatia katika kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Nyamhanga alitiwa hatiani juzi katika hukumu iliyosomwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Stanley Mwakihaba, kwa kosa la kumpora Sh. milioni 2.5 pamoja na simu ya mkononi Peter Mbwera kisha kumjeruhi kwa panga.

Akimsomea hukumu hiyo, Hakimu Mwakihaba alisema mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na kumkuta na hatia.

Aidha alisema hukumu hiyo ya miaka 30 jela itakuwa fundisho kwake na kwa watu wenye nia ya kuendelea kutekeleza matukio ya namna hiyo katika jamii.

Wakili wa Jamhuri, Janeth Kisibo, awali alidai kuwa Novemba 25, 2022 majira ya saa 2:00 usiku, mshtakiwa akiwa na panga, alimvamia Peter Mbwera na kumjeruhi kisha kumpora fedha na simu ya mkononi aina ya Tecno yenye thamani ya Sh. 80,000.

Kutokana na shtaka hilo, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya uhalifu wa namna hiyo na unaofanana nao.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo iliwahukumu vifungo vya miaka 20 watu wanne, wafanyakazi wa duka la vifaa vya ujenzi, mali ya Agnes Mwita.

Kutokana na hukumu hiyo, kila mmoja alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka mitano jela baada ya kukutwa na hatia ya kuvunja duka na kuiba mali yenye thamani ya Sh. milioni 277.4. Kadhalika, gari lililotumika katika wizi huo, lilitaifishwa kwa ajili ya kufidiwa sehemu ya mali walizoiba.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Mwakihaba alisema watuhumiwa hao wakimaliza kifungo watatakiwa kumlipa fidia mlalamikaji gharama za mali iliyoibiwa kutoka katika duka lake.

# Wasioona waibua suluhu, kilimo chenye tija

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha Wasioona Mkoa wa Shinyanga kimebainisha suluhisho la kudumu katika kilimo cha biashara na chakula ambalo litawasaidia wakulima kujikita zaidi katika kilimo chenye tija na faida.

Chama hicho kinachotekeleza mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma zilizotolewa kuboresha huduma za kilimo (PETS) chini ya ufadhili wa The Foundation for Civil Society katika kata sita, kimesema suluhisho la kudumu ni wakulima kuacha kudharau ushauri wa kitaalamu.

Akizungumza juzi katika kikao kazi cha kuweka mikakati ya uendelevu wa miradi ya PETS, Mwezeshaji wa Mradi huo, Dickson Maganga, alisema kuna sababu saba zinazofanya wakulima wa mazao ya chakula na biashara kushindwa kuzalisha mazao kwa wingi.

"Sababu hizo ni kutokuzingatia ushauri wa kitaalamu kwa kisingizio kuwa wanalima kwa kufuata utaalamu unawazidishia kazi nyingi shambani, wakulima kutokuwa na utamaduni wa kununua mbolea licha ya serikali kutoa mbolea ya ruzuku," alieleza.

Alitaja sababu zingine kuwa ni matumizi mabaya ya ardhi na kutokuwapo kwa mpangilio bora wa matumizi ya ardhi hasa maeneo maalumu kwa ajili ya kilimo na mifugo ingawa si kwa kiwango kikubwa na inafanya kukosekana kwa mazao mengi wakati wa mavuno.

"Sababu nyingine ni pamoja na kutokuwapo kwa mashamba darasa. Baadhi ya wakulima hawatumii mbolea za viwandani kwa madai kwamba zinaharibu ardhi na kuendelea kutumia samadi na upungufu wa maofisa ugani," alisema.

Ili kuondokana na hayo, alishauri kuwa ni vyema serikali ikawekeza kwenye kilimo hasa kwa kuagiza pembejeo kwa wakati, maofisa ugani wa kata kuwafikia wakulima na kuwashauri namna ya kulima kisasa, kuchimba visima virefu na mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili kuondokana na kutegemea mvua.

Katika kata hizo sita za Igunda, Kinamapula, Nyandekwa, Bukomela, Didia na Tinde, zaidi ya wakulima 16,000 wamefikiwa na mradi huo kwa lengo la kuhakikisha kilimo kinaendelea kuwa kiinua mgongo kwa mkulima na taifa kwa ujumla.



Ukurasa 12

## Janga la uraibu wa kamari linavyokuwa pasua kichwa

BUFE
IJUMAA AGOSTI 4, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Wamachinga Temeke sasa ni masoko tu waambiwa kuuzia barabarani ni kizamani

Ukurasa 12

# Jicho la TAFORI viwanda vya bidhaa za misitu, ni kuviongeza mara dufu

## •Jitihada kuhusu miti inayotoweka zaimarishwa

**Na Christina Haule, MOROGORO**

TAASISI ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), imeazimia kuongeza idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya misitu kutoka 650 hadi 1,500 katika kipindi cha miaka saba ijayo.

Ni baada ya kuweka mpango mkakati ambao utaimarisha huduma za misitu kwa jamii na kwamba hadi ifikapo mwaka 2030 viwanda hivyo vinatarajiwa kuongezeka na kuimarika ili kutoa ajira, kuchangia pato la taifa na kubadilisha maisha ya watanzania, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa TAFORI, Dk. Revocatus Mushumbusi.

Katika mahojiano ya Nipashe yanayofanyika mjini Morogoro, anasema katika mwaka wa fedha 2022/2030 taasisi inakusudia kufanya tafiti tano za kufanikisha kimkakati huo kwa lengo la kuboresha huduma za misitu kwa jamii ikiwamo kutathmini rasilimali za misitu na kuongeza tija katika viwanda vinavyotegemea malighafi kutoka misituni.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAFORI anasema taasisi imeweka mpango mkakati ambao utaimarisha huduma za misitu kwa jamii na kwamba hadi ifikapo 2030 viwanda vya kuchakata mazao ya misitu viwe vimeongezeka kutoka 650 hadi kufikia 1,500.

Anasema tayari wameshafanya tathmini ya viwanda hivyo ili kuvipatia malighafi kama inavyotakiwa ambapo tathmini ya awali imefanyika katika mikoa ya kusini na kubaini uwepo wa viwanda vya mazao hayo ya misitu kuwa ni 592 katika eneo hilo pekee.



Moja ya kiwanda cha kuchakata mazao ya misitu kilichopo mkoani Ruvuma, kinachosindika magogo ya mti wa msekeseke. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Mkurugenzi Mushumbusi anasema viwanda hivyo 592 vya mikoa vinapatikana Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Rukwa na vinashughulika na kuchakata bidhaa zinazotokana na uhandisi wa mazao ya misitu, vingine vinatengeneza karatasi, kutengeneza mkaa mbadala na vya kuzalisha umeme.

Anasema viwanda hivyo vinapata malighafi kwa asilimia 95 kutoka kwenye mashamba ya misitu ya serikali na watu binafsi yaliyoko maeneo mbalimbali.

Anaongeza kuwa tathmini hiyo imebaini kuwa bado kuna uchache wa misitu inayohitajika katika kulisha viwanda hivyo ambapo viwanda 592 ili vifanye kazi ipasavyo vinapaswa kupata misitu yenye ujazo mita milioni 4.5 kwa mwaka wakati kiasi kinachopatikana kwa sasa ni milioni 1.5 kwa mwaka sawa na asilimia 34 pekee ya uwezo uliopo wa kuvilisha .

Anasema zipo hekta 207,320 ambazo zina miti wakati asilimia 75 ya miti hiyo yote ni jamii ya misindano.

Anatoa rai kwa wadau wa misitu kuona haja ya namna ya kuendelea kuanzisha mashamba ya kuzalisha miti ya kutosha ili kulisha viwanda 592 vilivyopo katika kanda moja ya kusini pekee ambayo ni ya awali wakati tafiti zikipangwa kuendelea katika kanda nyingine nchini.

Mkurugenzi huyo anasema pia TAFORI inafanya tafiti ya pili ambayo ni kutathmni mchango wa sekta ya misitu katika pato la taifa kwa kutumia utafiti wa kijani ambao mpaka sasa mchango wa sekta ya misitu katika pato la taifa ni asilimia tatu hadi nne.

Anasema utafiti huo uliofanyika mwaka 2021/22 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wa vyuo vikuu vya UDOM na Chuo kikuu cha Sokoine wakitazama vitu vinavyohusika na mazao ya misitu kama mbao, nguzo, mkaa, nta, samani na asali kwa lengo la kupandisha mchango wa sekta misitu.

Dokta Mushumbusi anasema pia utafiti mwingine ni kutathmini idadi ya miti, masoko na namna ya kuzalisha miti ambayo ipo hatarini kutoweka akitaja jamii za msandali, msekeseke na mkulungu.

Anasema miti jamii ya miseseke na mikulungu hutumika katika uzalishaji wa mbao za kiwango cha hali ya juu ya daraja la kwanza wakati msandali hutumika katika kuzalisha manukato.

Anafafanua kuwa miti hiyo imepungua sana kutokana na miti hiyo kuota katika mazingira ya misitu ya asili na uvunaji wake kufanyika kwa uharibifu sababu wanavuna kuanzia mizizi.

Dokta Mushumbusi anasema wataendelea na utafiti kujua kiasi cha miti iliyopungua na kiwango kilichobaki msituni na hali ya soko ikoje na mwisho wa yote watumie mbinu gani kuhakikisha wanazalisha miti hiyo ili kuziba pengo.

Anasema utafiti umewaongoza katika mikoa ya nyanda za juu kusini na kubaini kiasi cha miti kilichopo hakitoshi ambapo tayari wameanza kukusanya vipando vya maabara na bustanini na kuanza kupanda miti hiyo , kuitunza kwa nia ya kuifikisha kwenye mashamba.

"Kazi yetu kubwa katika miti yote ni kuhakikisha tunaizalisha kadri tunavyoweza kupata vipando vya kutosha na pengine ifike mahali tuweze kuvisambaza kwa wananchi na tufanikishe kuanzisha mashamba maalum badala ya kutegemea miti hiyo kuipata katika mashamba ya asili peke yake" anasema.

Hivyo , anasema utafiti umeonyesha kuwa ipo miti mingine yenye ubora unaofanana na hiyo ambayo bado haijatambulika zaidi kuweza kutumika na kuwa mbadala wa jamii hiyo inayotishiwa na hatari ya kutoweka.

Inaendelea Uk 12

FEDHA

# Janga la uraibu wa kamari linavyokuwa pasua kichwa

•Huenda kila senti itatumika kubeti udhibiti na sheria kali ni muhimu kuokoa kizazi

**Na Gaudensia Mngumi**

SUALA la mmomonyoko wa maadili hasa lile linalohusu mapenzi ya jinsia moja, linatikisa taifa na kila anayepanda jukwaani, analikemea, ila chini ya zulia kuna jingine lililofichwa, ndiyo michezo ya kamari.

Zama hizi, Watanzania wanaifahamu kama 'kubeti' au 'betting' ambayo athari zake hazijasikika kwenye kipaza sauti lakini huenda ni mparanganyiko na mmomonyoko wa kila kitu.

Mahojiano na wanaobeti jijini Dar es Salaam (majina tunayo), wanasema ni biashara 'nzuri' inayojenga uraibu au uteja wa kucheza kamari kila unapopata pesa.

Wanasema uteja huo unasababisha matatizo ya fedha mfukoni, kwa kuwa kila pesa unayoishika mkononi unawaza kuielekeza kwenye kamari.

Wanakiri inaweza kuharibu uhusiano na hata kuvunja ndoa kwa kuwa kipato chote cha familia kinaweza kuelekezwa huko kuanzia mshahara, faida za biashara, kodi na makusanyo mengine mtu anayoyapata kwenye vitega uchumi vyake.

"Mwisho huenda kukawa na tatizo la afya ya akili kama vile katika baadhi ya matukio, unaweza kutumia fedha nyingi ili kupata mamilioni na badala yake ukaambulia sifuri. Kama ilivyotokea kwangu," anasema mmoja wao.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, Askofu William Mwamalanga, anasema michezo hiyo inaandaa mambo mengi ambayo yanaweza kuongeza uhalifu.

"Hii inaweza kuwa aina nyingine ya uhalifu na shughuli ambayo inachangia matendo hatari kama wizi, ujambazi na hata mauaji ili kupata fedha za kucheza kamari." Anasema.

Anatoa mfano wa muuza duka aliyeajiriwa anaweza kuiba fedha na hata kufilisi kwani kila siku anachukua pesa ili akabet. Anaweza kumaliza hata 5,000,000 kwa muda mfupi lakini asipate kitu.

Anasema lakini pamoja na hayo hasara nyingine ya michezo ya kamari kusababisha wizi miongoni mwa vijana, mfano wanaweza kuiba mifugo kama kuku, mbuzi, mayai, vifaa na vyombo nyumbani kama mapipa, mbao na akacheze kamari hiyo au kubeti.

Kiongozi mwingine wa dini ambaye hakutaka jina lake litajwe anasema wapo baadhi ya watumishi wa makanisa ambao hutumia fedha hizo kubet na kuna mikasa kama hiyo imesharipotiwa.

Anaeleza kuwa viongozi wa makanisa walitumia fedha kubet na kusababisha mparanganyiko na waumini kutamani kumchukulia hatua.

"Si hayo hata watumishi wa umma na taasisi binafsi na za kiraia wanatumia pesa kubet jambo ambalo ni hatari kwenye jamii hata kama athari hazitatokea au kuonekana leo."

"Si busara watu wanaishi vijiweni wakitegemea kupata pesa kupitia kamari, itafika kipindi wataiba hata kunyang'anya ili mradi wapate za kucheza kamari,"anasema.



**VYUO VIKUU**

Katika vyuo vikuu wasomi nao hawajaachwa nyuma kwenye 'betting' wanakiri kuwa wamo na wanapopewa fedha wengi wanazielekeza huko.

Wanasema kwa kila mwaka wa masomo wanapokea fedha ya chakula na malazi wanazoziita 'boom' takribani 500,000 inayotolewa kila baada ya miezi miwili na kwa mwaka zinatolewa mara nne hivyo kujikusanyia 2,000,000.

"Hata wanafunzi wa vyuo vikuu wakipewa mikopo ambayo inajumuisha fedha za chakula, bweni na za vitabu na daftari hutumiwa kubet." Anasema mmoja wao.

Anaeleza kuwa vyuoni wasomi hupata fedha za mikopo kwa ajili ya kazi za kujifunza kwa vitendo inayofikia Sh. 300,000, fedha za vitabu 200,000 ambazo baadhi wanazitumia kubet.

Anaongeza kuwa inawezekana kutumia fedha hizo vibaya kukawa na athari kwa wahusika na kunaweza kusababisha mapigano vyuoni, kujeruhi, wizi na hata kushindwa masomo.

**KASI YA KUBET**

Ufuatiliaji wa gazeti hili unabaini kuwa mabadiliko ya kiuchumi na ukosefu mkubwa wa ajira kwa vijana umefanikisha kupenyeza kamari katika nchi nyingi za Afrika ikiwamo Tanzania.

Licha ya kwamba kamari iliharamishwa miaka ya nyuma na kupewa majina mabaya kama karata tatu, korokoro na michezo ya kete imeendelea kukubalika na kuruhusiwa kisheria.

Hapa nchini kisheria ipo Bodi ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha-Bahati Nasibu ya Taifa, pia zipo bingo, kutumia sarafu au 'slots'na sasa ujio wa kamari za michezo (sports betting).

Leo kamari ni uwekezaji unaochochewa na maendeleo ya teknolojia hasa matumizi ya simu za mkononi yanayowezesha kupatikana na kuchezwa popote mijini na vijijini na simu zinaonyesha kuwa umeshinda au umeshindwa na malipo yanatolewa papo kwa papo.

Kamari ina masoko mapya mengi lakini kichocheo kikubwa ni ukosefu wa ajira na kiasi kikubwa hufanyika mitandaoni kamari ya mtandaoni hapa imekolea na inachochewa na kuongeza uwekaji fedha kidijitali huku wateja wakitumia simu, wengine mitandao ya intaneti, pamoja na malipo kufanyika haraka bila ubabaishaji yote huwaaminisha wateja na kuwavuta kucheza zaidi.

Wakati hayo yanatokea uraibu unafanya watu wengi kuadhirika maana kipato chote hukipeleka huko. Nguvu ya 'kubet' inaonekana kwenye mashirika ya kimataifa ambayo nayo yamo , timu kubwa za mpira duniani huko Ulaya nazo zinachochea.

Ongezeko la mapato kwa kiasi kikubwa linaongeza nguvu ya kamari, inasukumwa na teknolojia ya simu janja pamoja uaminifu ambao wateja wanahakikishiwa na kampuni zinazochezesha kwenye kutoa malipo kwa washindi.

Ingawa ukuaji wa sekta ya kamari Tanzania umetoa fursa za ziada za kuwa na kazi na mapato ya ziada ya kodi kwa serikali na hata kwa watu binafsi ni muhimu pia serikali kufahamu kuwa athari mbaya za kamari zipo kwenye afya na ustawi wa mtu binafsi, familia na taifa.

Umaskini na kukosa ajira, hasa miongoni mwa vijana unasababisha walalahoi kugeukia kamari kutokana na mitazamo kuwa ni chanzo cha mapato kinachowafaa , lakini hilo ni jambo endelevu? Wadau na serikali wajiulize na kufanya maamuzi.

Itakumbukwa kuwa Tanzania kamari ilikuwa haramu lakini ilianza kuhalalishwa kupitia kasino kwenye klabu za usiku na kuruhusu kuweka mashine za kamari kwenye baa, hoteli na mitaani. Hivi hakuna haja ya kufanya utafiti wa kuangalia athari za rukhusa hiyo na kuleta sheria kali?

Hata kama teknolojia imechangia kufikia kwa urahisi majukwaa ya kamari na kumwezesha kila mmoja kubeti na kupata fedha kwa muda mfupi baada ya kutangaziwa ushindi, hivi suala hilo ni endelevu kwa wananchi?.

**WATOTO HATARINI**

Nipashe inabaini kuwa zipo baadhi ya sehemu watoto hucheza kamari japo idadi yao si kubwa na pengine watu hawaitilii maanani lakini inaweza kuathiri watoto wa miaka 11 ambao bado wako shule za msingi.

Ikumbukwe kuwa, baadhi ya vichocheo vya kucheza kamari ni pamoja na ukosefu wa ajira, hali ngumu kiuchumi, kupenda starehe, shauku ya kupenda mpira wa miguu hasa wa Ulaya na ushawishi wa makundi rika.

Lakini kuwa na jamaa au wazazi wanaopenda sana kamari au kubeti kunaweza kuvuta wanafamilia wengine.

Matangazo ya biashara kwenye redio, runinga na mitandao ya kijamii bila kusahau kukua kwa teknolojia na serikali kuona kama njia ya kukusanya kodi na mapato. Hata hivyo ni mambo yanayohitaji kutungiwa sheria mpya na udhibiti mkali.

**ATHARI ZIJAZO**

Wasiwasi ni kwamba vijana wengi hushiriki katika kucheza kamari kwa kusababisha hasara ya kifedha kwao kibinafsi au familia, mwajiri au biashara zao na kwamba matokeo yake yanaweza kusababisha matatizo mengi.

Ni kama kukosa chakula lishe duni, kuvunjika uhusiano, kukwama kielimu, kuchanganyikiwa, ugomvi uhalifu na mwisho ni msongo wa mawazo na hata kifo.

Watoto wenye miaka 11 na 16 kucheza kamari ni hatari ni 'maambukizi' ya uraibu usiotibika.

Kwanza wanachezea kamari mtandaoni, wanaangalia masuala ya mmomonyoko wa maadili moja kwa moja yote hayo yanaongeza na kuchochea ushiriki mkubwa katika shughuli za kamari licha ya kuwa ni wadogo.



Michezo ya kamari katika sehemu mbalimbali .**PICHA: MTANDAO**

## JICHO LA TAFORI VIWANDA VYA BIDHAA ZA MISITU, NI KUVIONGEZA MARA DUFU

**INATOKA UK 11**

Akizungumzia mauzo ya miti anasema mauzo yanategemea na umri wa uvunaji na kwamba mwaka 2022/23 ujazo wa uvunaji uliongezeka kwa mita 600 katika shamba moja la Sao Hill.

Hivyo anasema awali miti huvunwa kwa miaka 25 na kuendelea ambapo watu wengi waliamini miaka 25 ni mingi na hawawezi kuwepo na kushindwa kupanda miti huku wakijisahau kuwa hata wao wanatumia miti waliyopanda wenzao waliowatangulia.

Anasema baada ya kupunguza umri wa uvunaji miti kutoka miaka 25 hadi kufikia miaka saba hadi 18 wananchi wengi wameendelea kuhamasika na kuchukua miti na kupanda kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo kupata nguzo, mbao na samani .

Aidha, mkurugenzi huyo anataja tafiti nyingine kuwa ni ufugaji nyuki ambao anasema shughuli za ufugaji wake ni fursa kwa wananchi na ambayo inaweza kuwaongezea kipato. Halikadhalika, anasema nyuki ni muhimu kwa kuwa wanachavusha mazao shambani ambayo bila nyuki baadhi ya yakiwemo alizeti yasingeweza kuendelea na kuleta manufaa.

Anakumbusha kuwa TAFORI ilianzishwa mwaka 1980 ikiwa na majukumu ya kufanya tafiti kuhusu rasimali za misitu na ufugaji nyuki nchini kupitia sheria namba 5 sura namba 277 ambayo imetimiza miaka 43 kwa sasa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kama vipi chupa ya chai ivunjwe tutumie mabakuli





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

IPO hadithi ya mtoto mharibifu, aliyekuwa na tabia ya kuharibu vifaa nyumbani, kiasi cha kumfanya mama yake kuwa kama kichaa akimlinda kila wakati.

Hali iyo ilimfanya mtoto kuishi kwa wasiwasi, huku akipendelea sana kuwa karibu na chupa ya chai, ambayo ilihusika katika kumtunzia uji na maziwa na kila mara akihatarisha kuivunja.

Mama naye aliingiwa na wasiwasi kuwa endapo chupa hiyo itavunjika atafanya nini, wakati hali yake kiuchumi ilikuwa duni, hivyo asingemudu kununua nyingine.

Mara zote akawa mtu wa kukemea, akijua ikitokea akakaa mbali huyu mwanawe, bila shaka maisha ya chupa ile yatakuwa shakani na hatapata nyingine.

Kwa kuwa sasa ilionekana kero kwa mtoto yule, siku moja akapata wazo la kumaliza wasiwasi aliokuwa nao, nalo likawa la kuivunjilia mbali ili isiwepo tena na kelele za mama ziishe.

Kweli, siku moja alipoamka na kupata kifunguakinywa chake kama kawaida kupitia chupa ile, mama aliaga kwenda sokoni kununua mahitaji ndipo mtoto akaona huo ndio ulikuwa wakati mwafaka.

Aliivunjilia mbali chupa ile, na mama aliporudi akakutana na vipande vipande na alipohoji kwa hasira, mwanawe alilia na kumwambia hakuwa na jinsi, ila kuondokana na udhia ule.

Kuanzia siku hiyo, nyumba ikawa ya amani licha ya sasa uji, chai na maziwa kuhifadhiwa na kunywewa kwenye vikombe na mabakuli na hatimaye kila kitu kikasahaulika na maisha yakaendelea.

Nimemsikia takriban mara tatu, nne hivi, Mama, Chifu Hangaya, Rais Samia Suluhu Hassan, akililia amani na utulivu wa nchi na hasa kuchelea Watanzania kugawanyika kutokana na jambo, mtu au kikundi cha watu.

Kilio chake kinapaa zaidi kutokanana muktadha wa kelele za mkataba wa ushirikiano wa Serikali za Tanzania na Dubai, kuhusu uwekezaji kwenye bandari za Tanzania.

Anaona kama tunavyoona sisi, kwamba kuna mgawanyiko unaolemea Watanzania wanaojadili mkataba huo,katika nyanja na medani mbalimbali wakiwapo wanaopinga mkataba, wanaounga mkono na wasio na msimamo.

Kuna mgawanyiko wa kimsimamo na kimawazo, baina ya wanasiasa, wataalamu, wanahabari, viongozi wa dini na wanasheria, kila upande ukivutia ngozi kwake kwa sababu dhahiri na fiche.

Jina maarufu linalobamba miongoni mwa ndimi za jamii ya Watanzania ni DP World, kampuni inayopigiwa upatu na kupingwa kuwekeza katika bandari nchini.Uzuri ni kwamba makundi yote hayo hakuna linalopinga uwekezaji.

Bali katika makundi hayo, kuna wanaohoji mkataba na vipengee vyake, lakini wapo wasiotaka kujishughulisha na mkataba ila DP World apewe tu hatakama ni bandari zote, zikiwamo za mabwawani.

Bila shaka Chifu Hangaya pia ametishwa na jinsi matusi yanavyorushwa hovyo na watu bila kujali rika, utadhani wamevutishwa bangi. Mdogo anamtukana mkubwa bila kujali na mkubwa anamwaga mitusi bila aibu wala hofu!

Kwa halihiyo, mama yeyote mwenye dhamana ya kuangalia wanawe akitaka waishi pamoja kwa mshikamano thabiti, lazima atasimama na kukemea hali hiyo isiyo na siha, kwa mustakabali mwema wa familia, ukoo na Taifa kwa ujumla.

Lakini ili kuondokana na sintofahamu hiyo, Watanzania wachache miongoni mwetu, wakaona ni bora kwenda mahakamani kuangalia ni nini hasa kilichomo kwenye mkataba na kama kinaweza kufafanuliwa na kueleweka ili kuondoa mtanziko uliopo.

Ni bora mahakama ikavunja chupa hii, ili tuondokane na taharuki iliyopo hivi sasa, kwa sababu hakuliki, hakulaliki hivi sasa kisa ni mkataba-chupa iliyoko mikononi mwa mtoto.

Watu wanataka kujua; je, uwekezaji huu unaungwa mkono na kila Mtanzania? Kusainiwa, kuwasilishwa bungeni na kuridhiwa kwake kulishirikisha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Rasilimali na Maliasili?

Je, kulishirikisha Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba inayohusu Raslimali na Maliasi za Nchi? Umma uliarifiwa na kupewa muda mwafaka kushiriki na kutoa maoni yake?

Je,zile ibara 14 za mkataba wenyewe zinakiuka ibara zile tatu za Katiba ya Tanzania? Na ibara mbili za mkataba zinakiuka kile kifungu kimoja cha Sheria ya Mikataba ya Tanzania?

Kama haitoshi, je, makubaliano kati ya Tanzania na Dubai (IGA) yalifuata taratibu za kisheria, kuchagua njia ya ununuzi ambayo iko chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Uuzi wa Umma? na,

Vinginevyo Mama avunje tu chupa ya chai ili tuendelee namaisha yakunywea kwenye vikombe na mabakuli. Alamsiki!

BIASHARA

# Wamachinga Temeke sasa ni masoko tu waambiwa kuuzia barabarani ni kizamani

## •Mkurugenzi atamba yapo yakutosha, haachwi mtu



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi (mwenye kipaza sauti), akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo baada ya kulikagua. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

BIDHAA kupangwa pembeni mwa barabara, vituo vya mabasi, njia na madaraja ya wanaotembea ni matokeo ya fikra kuwa ndiko wateja na biashara iliko.

Mazoea hayo yamesababisha wamachinga kuvamia sehemu hizo karibu nchi nzima na kudaiwa kuwa wanavuruga taratibu za mipango miji na matokeo yake ni kupambana na wanamgambo wa miji na majiji kila uchao.

"Sasa tukianzia na Temeke tunataka kumaliza mazoea hayo na kuondoa dhana waliyonayo kwamba pembeni mwa barabara ndiko biashara iliko, ili waende kwenye masoko rasmi." Anasema Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke-Dar es Salaam, Herihuruma Mabelya.

Anaongeza kuwa Temeke imeazimia kuchukua kila hatua ili wamachinga wanaofanya shughuli zao pembeni mwa barabara na maeneo mengine yasiyo rasmi wanafanya biashara masokoni.

Anakumbusha kuwa serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa masoko, lakini kutokana na dhana hiyo kuwa barabarani ndipo walipo wateja wanayakwepa.

"Tunachukua hatua hiyo kwa kuwa masoko 25 yaliyopo katika manispaa yana miundombinu muhimu na uwezo wa kuchukua wamachinga wote 9,500 wa Temeke na wakafanya biashara zao bila bugudha." Anasema .

Katika mazungumzo yake na gazeti hili mara baada ya ukaguzi wa ujenzi wa soko jipya la Mbagala Zakhiem hivi karibuni, anaongeza kuwa kinachofuata sasa ni kuwaondoa wote wanaoendelea kufanya biashara barabarani na sehemu zisizo rasmi.

"Tutaanzisha msako wa usiku ili pasiwepo na wamachinga wanaozagaa pembeni mwa barabara. Tumebaini kuwa mchana hawapo barabarani, lakini usiku wanakuja kufanya biashara ni lazima tuweke mipango rasmi," anaongeza.

Manispaa hiyo imepanga wamachinga wafanyie biashara zao katika maeneo bora na salama, badala ya kuwa kandokando ya barabara na kuhatarisha maisha yao lakini kuchafua mazingira, anasema.

Aidha, anafafanua kuwa Temeke ina zaidi ya wafanyabiashara 20,000 wakiwamo wamachinga, wenye gereji, maduka, mama na babalishe na kwamba katika mwaka huu wa fedha wataongezeka hadi kufikia 30,000.

"Tumetenga Shilingi bilioni moja ambazo zitatumika kwa ajili ya ukarabati wa masoko ndani ya manispaa yetu, ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kila soko lina huduma muhimu na za msingi ili wamachinga wasiwe na kisingizio cha kuyakwepa," anaonya.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi anamuagiza mkandarasi wa ujenzi wa soko la kisasa lililopo Mbagala Kibonde Maji la Zakhem, kulikabidhi kwa manispaa ifikapo Agosti 15 mwaka huu.

Vilevile, Matinyi anawageukia viongozi wa manispaa hiyo kusimamia mgawanyo wa vizimba vya biashara kulingana na ukubwa wa biashara na kwamba kuna vizimba 160.

Anaagiza kuwa baada ya manispaa kukabidhiwa soko hilo, mkurugenzi na meya na katibu wa wafanyabiashara wa soko hilo watakutana kupanga namna wafanyabiashara watakavyo pangwa ndani ya soko huku kipaumbele kikiwa ni kwa wale wafanyabiashara waliokuwapo awali.

Katika ufafanuzi zaidi wa ujenzi wa soko hilo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Mabelya anasema kutakuwa na ofisi za manispaa ambazo zitasimamaia masuala ya wafanyabiashara na miundombinu.

"Lakini pia kutakuwa na kitengo cha TEHAMA ambacho kitakuwa na mitambo maalumu ya kufuatilia wafanyabiashara na utendaji kazi ndani ya soko," anasema.

**WAHUNI KUADHIBIWA**

Mabelya anasema hatua zitachukuliwa kwa wafanyabiashara ambao watafanya uhuni endapo watapangishwa kwa fedha kidogo ya serikali kisha nao wakapangisha wengine kwa gharama kubwa, hao ni lazima watawafuatilia na kukomesha mienendo hiyo.

Anakumbusha kuwa ujenzi wa soko ulianza mwanzoni mwa mwaka 2022 mkandarasi anayejenga ni Group Six International Limited,

Msimamizi wa ujenzi huo Hans Charles anasema kazi imekamilika na kwamba wapo kwenye hatua za mwisho.

Mmoja wa wafanyabiashara watakaoingia katika soko hilo, aliyejitambulisha kwa jina la Veronica Bunde, anasema awali pamoja na wenzake walidhani si miongoni mwa watakaofanya biashara humo.

"Sisi tulikuwa tukiuza nyanya hapa hata kabla soko halijavunjwa na kujengwa upya, lakini kulikuwa na taarifa kwamba watakuja wafanyabiashara wengine, hivyo tukajua tumeachwa," anasema Veronica.

Anarejea ufafanuzi wa mkurugenzi wa manispaa hiyo kwamba wale waliokuwapo tangu awali ndiyo watapewa kipeumbele kwanza, akisema umewatia moyo na maelezo hayo na sasa anajiandaa kuanza biashara mara soko litakapozinduliwa na kufunguliwa.





# Bilioni 35/- kuboresha kilimo cha umwagiliaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imetenga zaidi Sh. bilioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji mkoani Singida ili kuongeza uzalishaji na tija kwenye sekta ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye viwanja vya maonyesho ya wakulima Kanda ya Kati Nzuguni jijini Dodoma.

Alisema skimu ya msingi iliyoko wilaya ya Mkalama yenye ekari 2,000 itajengwa kwa gharama ya Sh. Bilioni 34.17 na Sh. bilioni 1.8 zitatumika kuanza shughuli za awali za ujenzi wa skimu ya Tyame wilaya ya Iramba yenye ekari 4,000.

Serukamba alisema miradi mingine itakayoanza kutekelezwa katika mwaka 2023/24 mkoani Singida ni pamoja na skimu 15 zenye jumla ya ekari 13,833 ambazo zitafanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi, skimu 12 zenye jumla ya ekari 7,285 zitafanyiwa upembuzi na ukarabati, mabwawa sita yatafanyiwa upembuzi yakinifu usanifu na ujenzi ambayo yatamwagilia eneo lenye hekta 4,900.

"Tunaratajia kuwa baada ya kukamilika baada ya utekelezaji wa miradi mkoa utakuwa na eneo lenye jumla ya hekta 32,018 za umwagiliaji sawa na asilimia 65.85 zenye eneo lote la hekta 47,000 zinazofaa kwa umwagiliaji zilizopo na wakulima 80,045 watakaonufaika," alisema.

Pia alisema matumizi ya pembejeo za kilimo na ufugaji yanasisitizwa ili kuhakikisha kuwa tija ya uzalishaji inaongezeka, katika kipindi cha mwaka 2022/23, tani 395.38 za mbegu za alizeti ruzuku ya serikali ya Sh.bilion 3.1 zilizopelekwa na kutumika na wakulima.

"Aidha mbolea yenye ruzuku ya serikali kiasi cha tani 2,973 zenye thamani ya Sh. bilioni 4.1 zilizopokelewa na kutumika na wakulima, katika sekta ya mifugo jumla ya lita 2,664 za madawa ya kuogesha mifugo zenye thamani ya Sh.milioni 119.8 zilizopokelewa na kutumika na wafugaji,"alisema Serukamba.

# CCM yataka wazee, watoto kusamehewa kazi TASAF

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida kimeuagiza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuweka utaratibu mzuri wa kuwasaidia watoto yatima na wazee wasiojiweza badala ya kuwataka wafanye kazi zikiwamo za kuchimba mitaro na malambo ili wapewe fedha.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Rungwa kwenye mkutano wa hadhara.

Katika mkutano huo, baadhi ya wananchi walilalamika kuwa TASAF imekuwa na tabia ya kuwataka watoto yatima na wazee ambao ni walengwa, wafanye kazi kwanza ili wapewe fedha.

"Ni kweli kwenye maeneo mengine unakuta mtu anaandikishwa TASAF hana hata nguvu anaambiwa kwenda kuchimba mtaro. Angekuwa na nguvu si angechimba kwake au kufanya kibarua apate hela? Kama tunawasaidia watu tuwasaidie sasa hili la kutaka hata watoto yatima wafanye kazi haliko sawa," alisema.

**Niwahakikishie, nimeyaona, nimeyachukua mwenyewe naenda kumwambia aliyewateua kuhusu mambo yanavyoendelea na namna ambavyo sijaridhika na utatuzi wa changamoto ya maji.**

Mlata alisema viongozi wanaosimamia TASAF lazima watambue kuwa mfuko huu ni kwa ajili ya kusaidia watu wasiojiweza hivyo uwekwe utaratibu mzuri wa kuwatambua na kuwasaidia na kama wapo wenye nguvu na wameomba kuingizwa katika mpango huo watenganishe ili wao ndio wakafanye kazi hizo.

Kuhusu kero ya maji iliyolalamikiwa na wananchi wa kijiji cha Rungwa, mwenyekiti huyo aliiagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Halmashauri ya Itigi kufika katika kijiji hicho ndani ya wiki hii na kulipatia ufumbuzi tatizo la maji.

Akifafanua hoja ya TASAF, Ofisa Tarafa ya Itigi, Eliutha Kidenya, alisema walengwa wanaohudumiwa na mfuko huo huwa wanapewa nafasi kupitia mikutano ya ngazi za vijiji kuibua miradi hivyo baadhi ya miradi wanayoiibua wanaotakiwa kufanya kazi ni walengwa wenyewe.

Alisema katika kata ya Rungwa katika baadhi ya vijiji baadhi ya walengwa walijiandikisha kwamba wana watu wa kwenda kufanya kazi lakini kihalisia kwenye utekelezaji wengi hawawezi na kwamba kutokana na changamoto hiyo katika awamu ya pili ya TASAF wasio na uwezo hawashirikishwi kwenye kazi hizo.

Hivi karibu wakati wa Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ilitokea taarifa kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Mkoa wa Singida katika kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini umetoa fedha za ruzuku Sh. bilioni 9.2 kwa walengwa 134,275 wa vijiji 592 hadi kufikia Juni 2023.

Katika kaya za walengwa hao watoto 18,465 waliochini ya miaka mitano na watoto 59,230 wanaosoma shule za msingi na Sekondari pia wamenufaika na ruzuku hizo.




Mkurugenzi wa Elimu Maalumu Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonolojia, Dk. Magreth Matonya, akizungumza na washiriki wa kikao cha tathimni ya utekelezaji wa mradi wa uboreshji maisha ya watu wenye ulemavu kwenye sekta ya elimu unaotekelezwa na shirika la Foundation for Disabilities Hope (FDH) kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS), wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa shirika hilo, Michael Salali. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Serikali yataka utafiti vikwazo elimu watoto wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imemwagiza ofisa elimu maalum wa wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma kubaini vikwazo vyote vinavyokwamisha watoto wenye ulemavu kupata elimu ili vipatiwe suluhu.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum wa Wizara hiyo, Dk. Magreth Matonya, alitoa agizo hilo jana wilayani hapa kwenye kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji maisha ya watu wenye ulemavu kwenye sekta ya elimu. Mradi huo unatekelezwa na shirika la Foundation For Disabilities Hope (FDH) kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society.

Alisema idara ya elimu maalum wilaya ya Mpwapwa inatakiwa kubainisha vikwazo mbalimbali ambavyo vinakwamisha jitihada za serikali pamoja na wadau wengine kusaidia watu wenye ulemavu kupata elimu.

"Watu wanawachukulia wenye ulemavu kama siyo watu nataka nipate changamoto zinazokwamisha walemavu kupata elimu ili waliopo nyumbani waweze kwenda darasani," alisema Dk. Matonya

Alisema baadhi ya vikwazo vilivyopo hivi sasa ni pamoja na miundombinu isiyo rafiki katika shule mbalimbali ambazo zinakwamisha wenye ulemavu kupata elimu.

"Zipo changamoto nyingi kwa walemavu ikiwemo miundombinu ya vyoo isiyo rafiki, madarasa yenye ngazi badala ya mseleleko, umbali wa shule lakini pia ukosefu wa viti mwendo kwa wenye ulemavu wa viungo ambavyo kama wilaya mtashikamana kwa kutushirikisha sisi haiwezi kuwa tatizo tena," alisema.

Pia alisema bado lipo tatizo la wazazi kufungia watoto wenye ulemavu ndani na kuwanyima haki yao ya kupata elimu kama ilivyo kwa wengine hivyo jamii inapaswa kubadili mtizamo huo ili kuwasaidia.

Alisema shule nyingi nchini bado hazina walimu wenye taaluma rasmi inayohusu elimu maalum hivyo kushindwa kuwahudumia watoto wengi wenye mahitaji maalum.

Kadhalika, aliwataka wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalum kushikamana ili kuwasaidia kupata haki zao za msingi kwani imekuwepo tabia ya baadhi yao kukimbia majukumu yao.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, Bruno Mwakibibi, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, alisema wameandaa mwongozo utakaotumika kuwabaini watoto wenye mahitaji maalum utakaosambazwa katika maeneo mbalimbali.

Awali, Mwenyekiti wa FDH, Michael Salali, alisema mradi huo unatekelezwa katika kata mbili ambapo tayari wamewafikia walimu 250 na kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum.

"Mradi wetu unalenga kuwezesha watoto wenye ulemavu kupata elimu na kuondoa tabia kwa jamii kuwaficha ndani na hadi sasa tayari tumeibua watoto 72 lakini pia tumetoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini, waganga wa jadi, kamati za shule, viongozi wa kisiasa hali ambayo imesaidia vikao vya vijiji kufanya elimu maalum kuwa ajenda yao ya kudumu kwenye mikutano," alisema.





# Mpango awapa somo watafiti mbegu wazawa

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

SERIKALI imetaka mbegu za mazao mbalimbali zinazozalishwa kupitia mikononi mwa watafiti wazawa kwa kuwa ndio wanajua mazingira halisi nchini.

Kutokana na hali hiyo, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kutumia watafiti wake kuongeza uzalishaji wa ndani ili kupunguza utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alitoa agizo hilo juzi alipotembelea banda la TARI kwenye viwanja vya Maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, maarufu kama Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye kwenye Viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

Dk. Mpango alisema dhamira ya serikali, kwanza ni kuwathamini watafiti wa ndani na kwa sasa inawaunga mkono ikiwamo kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 200 mwaka 2021 mpaka Sh. bilioni 970 mwaka 2023/24 ili kuongeza uzalishaji wa mbegu ambazo zinaendana na mazingira pamoja na udongo hatua inayoweza kumtatulia mkulima changamoto zake.

**Hivi mkulima wa kijiji cha Mayamaya kule Dodoma akitaka kujua elimu ya afya ya udongo wake je, hapa? Au lazima watalaam waende kupima kwanza?**

"Dhamira ya serikali kwa sasa ni kuwaunga mkono watafiti wetu ili waweze kuzalisha mbegu zitakazotokana kwenye vichwa vya Watazania na zinazoendana na mazingira yetu ya hapa nchini na tutawapa zawadi kutokana na mchango wao," alisema.

Dk Mpango alisema lengo la serikali ni kuona uzalishaji wa mbegu za ndani unakuwa mkubwa ili wakulima waamue na kuchagua aina gani za mbegu wanazoweza kuzitumia na si kuletewa kutoka nje ya nchi ambazo wakati mwingine haziendani na mazingira ya Tanzania.

Aidha, aliagiza elimu ya afya ya udongo ianze kutolewa na kufika kwa watu wote nchini ili kupunguza upotevu wa mbolea unaotumiwa holela na wakulima.

"Hivi mkulima wa kijiji cha Mayamaya kule Dodoma akitaka kujua elimu ya afya ya udongo wake je, hapa? Au lazima watalaam waende kupima kwanza? Tunataka hii elimu isambae kwa wakulima ili wapange kilimo gani wanaweza kulima kwa kutumia udongo wake kwa kuwa tunapoteza kiasi kikubwa cha mbolea ambazo zingeweza kutumika kwenye maeneo mengine," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema ramani zilizopo tayari zinaonyesha afya ya udongo kwa nchi nzima na tayari wakulima wameshaanza kunufaika ikiwemo kuamua mazao ya kulima baada ya kujua afya ya udongo kwenye mashamba yao.

" Kwa sasa mkulima anapokuja na kutumia anataka kufanya uwekezaji kwenye kilimo sehemu Fulani, tunamwambia ni lazima ajue afya ya udongo, hivyo tunatengeneza ramani mbalimbali zinazoonyesha afya ya udongo katika nchi ili kumwezesha kuchagua uwekezaji wa kilimo gani utakaoweza kumpa tija katika eneo hilo," alisema.

Dk Mkamilo alisema TARI tayari imeweka mikakati ya kuhakikisha inatoa elimu ya afya ya udongo kwa kuingia ndani zaidi kuanzia kwa wakulima walioko vijijini ili kufanya matumizi sahihi ya mbolea kwenye mazao watakayochagua.




Mtaalamu wa Mifumo kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara, Jastine Govela (kushoto), akitoa maelezo kwa baadhi ya madereva wa bodaboda wa Jiji la Mbeya, jinsi watumiaji wa vyombo vya moto wanavyochangia 263/- ya matengezo ya barabara kutoka katika kila lita ya petroli au dizeli wanayonunua na namna fedha hiyo inavyotumika kukarabati miundombinu ya barabara nchini, wakati wa maonyesho ya wakulima Nanenane kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini humo jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# JKT yapongeza serikali kwa uendelezaji vijana

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Tawi la Utawala Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Hassan Mabena, ameipongeza serikali kwa kuwaona vijana na kuwatengenezea mazingira ya kujiinua kiuchumi kupitia mradi unaolenga kuongeza ushiriki wao katika kilimo.

Mradi huo ni ule wa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko (Building a Better Tomorrow-BBT) ambao sasa utawahusisha na vijana wa kujitolea wa JKT.

Jenerali Mabena aliyasema hayo jana katika maonyesho ya wakulima, maarufu kama Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya yanakofanyika kitaifa kwa mwaka wa pili mfululizo.

Alisema katika mradi huo vijana watapata mafunzo katika vituo atamizi vya namna ya kufanya shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa tija na hivyo kuchangia katika uchumi wa Taifa na wao kumudu kuendesha maisha yao.

Jenerali Mabena alisema tayari Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Kilimo zimeshatia saini makubaliano na mpango uliopo sasa ni kurudia yale makubaliano ili kuwahusisha vijana wa JKT katika mpango wa serikali wa kuwa na mashamba nundu.

Alisema hivi karibuni Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa zitatia saini makubaliano ili vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT nao wahusishwe katika mpango huo maalum.

"Ili kuhakikisha mpango unawezeshwa serikali imetoa malekezo kwa taasisi za kibenki kupunguza riba za ukopaji na kutoa masharti nafuu ili wafugaji , wakulima na wavuvi waweze kuendeleza maeneo hayo ili kuongeza mazao ya chakula, ufugaji na uvuvi na pia itawezesha vijana kupata ajira, itakwenda kuongeza pato la Taifa na uhakika wa usalama wa chakula nchini." Alisema.

# NEMC yaonya uwekezaji bila vibali mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewakumbusha wawekezaji wa miradi kuhakikisha wanapata cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira kabla ya kuanza shughuli zao.

NEMC imesema vyeti hivyo ni takwa la kisheria kwa ajili ya kulinda uchafuzi wa mazingira, hivyo yeyote atakayebainika kukiuka sheria hiyo ajiandae kwa adhabu.

Ofisa Elimu ya Jamii wa NEMC, Suzan Chawe, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye maonyesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale, mkoani hapa.

Alisema NEMC imerahisisha mchakato wa kupata cheti cha tathmini ya mazingira kwani kwa sasa wawekezaji wanaweza kuvipata kupitia mfumo wa kielektroniki (online).

Chawe alisema huduma hiyo inapatikana kwenye ofisi mbalimbali za baraza zinazopatikana Tanzania nzima hivyo kuwashauri watu wanaotaka kuanzisha miradi kuhakikisha wanavipata kabla ya kuanzisha miradi.

"Pia tunawakaribisha wenye sifa za kuwa washauri elekezi wa mazingira kujisajili na kupata cheti cha utendaji kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari za mazingira na kufanya ukaguzi wa mazingira kwa ujumla," alisema.

Meneja wa NEMC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Josia Msomi, alitaja huduma zinazotolewa kwenye banda la NEMC kuwa ni usajili wa wataalamu elekezi wa Mazingira na usajili wa miradi kwa ajili ya cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira.

Alitaja shughuli zingine wanazotoa kuwa ni elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kupokea malalamiko na maoni kwa wananchi kuhusu masuala ya mazingira na kuyashughulikia.

"Tunawakaribisha wananchi, wadau wa mazingira na wawekezaji kwenye miradi mbalimbali waje kwenye maonyesho haya ambapo watasajiliwa kwa mtandao kupata huduma za baraza, wananchi watupe maoni ya nini wanachotaka tuboreshe," alisema

Alisema kuna hatua za kufuata ili kupata cheti cha tathmini ya athari za mazingira kwenye mradi ni usajili wa mradi husika kwa kujaza fomu maalum ya maombi ya usajili kwenda (NEMC).

Msomi alitaja hatua zingine kuwa ni fomu ya maombi iliyojazwa pamoja na muhtasari wa miradi iliyowasilishwa NEMC, kufanyiwa upembuzi ili kujua kama kuna haja ya kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira ama la.



## Mtaalamu aeleza mgawanyo wa nguvu kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Taasisi ya Wahandisi Wanawake Tanzania, Dk. Gemma Modu, amesema wanawake wanachukua nusu ya idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi za kiuchumi na nusu ya nguvu kazi ya nchi ya kiuchumi inachukuliwa na wanawake.

Akizungumza katika kongamano la taasisi hiyo lililofanyika visiwani Zanzibar ambalo liliambatana na maonyesho ya kazi za wahandisi, alisema ushiriki wao ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi lakini kiwango cha ushiriki katika kufanya kazi za kiuchumi ni ndogo kwa wanawake ikilinganishwa na wanaume.

Dk. Modu alisema kuna pengo la ushiriki wa jinsia ya kike katika ngazi na shughuli mbalimbali za maendeleo hasa zinazohusiana na sayansi na teknolojia na uhandisi.

Alisema takwimu za Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania (ERB) mpaka sasa ni asilimia 13 ya wahandisi waliosajiliwa na katika Taasisi ya Wahandisi Tanzania, kuna wahandishi karibu 4,000 lakini wanawake ni 300, sawa na asilimia saba.

"Takwimu zinaonyesha kuwa ushiriki wa wanawake katika uhandisi ni mdogo sana ukilinganishwa na wanaume na unahitajika kuimarishwa" alisema.

Aidha, alisema majukumu Taasisi ya Wahandishi Tanzania Kitengo cha Wanawake, lengo kutimiza malengo ya taasisi ikiwamo kukuza na kuendeleza fani ya uhandisi miongoni mwa wasichana na wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika nafasi za kujenga uchumi wa nchi.

Rais huyo alisema kwa mara ya kwanza kongamano hilo limefanyika Zanzibar na kwamba uhandisi una mchango mkubwa wa kuleta maendeleo katika yoyote ikiwamo Tanzania.

Kutokana na umuhimu huo, alisema katika miaka ya karibuni katika ngazi ya kimataifa na kitaifa, mikakati mbalimbali imeanzishwa ili kufikia maendeleo endelevu.

Pia alisema tathmini ya kazi ndogo zinazohusishwa na kazi na maendeleo endelevu kwa kiasi kikubwa zinategemea ujuzi na ubunifu katika sayansi na teknolojia na uhandisi ukiwa moja wapo.

# Mwinyi apongeza mchango wa wahandisi wanawake kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar zinatambua mchango wa wahandisi wanawake na zinathamini kazi za kihandisi wanazofanya.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la nane la Taasisi ya Wahandisi Wanawake Tanzania ambalo limefanyika visiwani hapa likiwa na kaulimbiu: "Nguvu ya Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Kihandisi."

Alisema serikali zote mbili zinafanya jitihada katika kushirikisha wanawake katika shughuli mbalimbali, kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kujiajiri, kuhamasisha utambuzi wa fursa kupitia rasilimali zilizopo, kurejesha stadi za ujuzi, elimu ya uanagenzi vyuoni na kutenga bajeti kwa ajili ya kufanikisha shughuli za utafiti na ubunifu.

Makangamano hayo, alisema yana mchango mkubwa katika kuunga mkono juhudi za serikali kuendeleza ubunifu wa kisanyansi na kazi za kihandisi ambazo huleta chachu katika maendeleo ya taifa.

Alisema hilo ni jambo jema na linalohitaji kuendelezwa kwa hakika linaongeza ari na hamasa ya wahandisi wanawake kufanya bidii katika fani hiyo.

> **Navipongeza sana vyuo na shule zilizojitokeza kushiriki katika maonyesho haya. Nimefarajika kuona Tanzania ilivyo na wabunifu wenye ubunifu wa kipekee unaoonyeshwa kwenye maonyesho haya.**

"Wito wangu kwenu wahandisi mwendelee kushirikiana ili kuhakikisha mnachangia vilivyo kwenye maendeleo ya nchi na hatimaye Tanzania kufikia malengo yake ya kuwa na uchumi wa juu wa kati ifikapo mwaka 2025," alisema.

Dk. Mwinyi alisema mkakati mzuri ni kuwahamasisha watoto wa kike kuweza kujiamini na kujiunga katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati na mpaka sasa takwimu zinaonyesha bado wanawake ni wachache kwenye uhandisi.

"Navipongeza sana vyuo na shule zilizojitokeza kushiriki katika maonyesho haya. Nimefarajika kuona Tanzania ilivyo na wabunifu wenye ubunifu wa kipekee unaoonyeshwa kwenye maonyesho haya. Nawapongeza sana kwa jitihada hizi," alisema.

Dk Mwinyi alisema Serikali inatambua mchango wa taaluma ya uhandisi na wahandisi wa fani mbalimbali katika ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia ukuaji wa huduma mbalimbali zikiwemo, ujenzi wa viwanda,

Aidha, alisema serikali itahakikisha inawasaidia vizuri wasichana wanaosoma masomo ya sayansi katika elimu ya sekondari, vyuo vya mafunzo ya amali na vyuo vikuu hatua ambayo itasaidia kuongeza idadi ya wahandisi wanawake nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Aisha Amour, akisoma hotuba ya waziri wa wizara hiyo, alisema serikali inatambua mchango wa taaluma ya uhandisi katika ukuzaji wa uchumi.

Alisema Tanzania ina wahandisi 35,000 wakiwemo wanawake 4,633 na kwamba hiyo ni idadi ndogo, hivyo kuna uhitaji wa kuwa na wahandisi wengi wanawake na kuna haja ya kuongeza ushawishi wa wanafunzi wa kike kusoma masomo ya sayansi na hisabati ili kuongeza idadi ya wahandisi wanawake.

Katibu mkuu huyo alisema serikali ya Muungano inathamini kazi za kihandisi na mchango wa wahandishi wakiwemo wanawake katika maendeleo ya nchi. Kwa kutambua shughuhi za kihandisi katika kuendeleza uchumi wa nchi, serikali imeandaa program ya kuwawezesha kwa kuwapa mafunzo vitendo.



Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Sakware akizungumza na waandishi wa habari Mkoa wa Mjini Unguja jana, kuhusu ukaguzi walioufanya wa vyombo vya moto sehemu mbalimbali za mkoa huo. Kushoto ni Meneja Mamlaka ya Bima Tanzania, Mohamed Khamis Ameir. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TIRA yaonya udanganyifu huduma za bima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imewataka mawakala wa bima kuacha kufanya udanganyifu katika kutoa huduma za bima kwa sababu kitendo hicho kinaikosesha serikali mapato.

Onyo hilo la TIRA limetolewa kutokana na kuifutia usajili wa huduma za uwakala wa bima kampuni ya Tabasam baada ya kubainika kukiuka sheria za kutoa huduma na majukumu ya huduma hizo kwa kufanya udanganyifu kwa wateja.

Kamishna Mkuu wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa kutokana na ukaguzi unaofanyika kwa mawakala na vyombo vya moto kwa mkoa wa Mjini Magharibi.

Dk. Saqware alisema kwa mujibu wa ukaguzi uliofanyika, baadhi ya mawakala wanakiuka masharti ya kutoa huduma kwa wateja kwa kufanya udanganyifu ikiwamo kukusanya fedha za malipo na kushindwa kuziwasilisha sehemu husika.

Alisema biashara ya bima inaongozwa na sifa mama ya kanuni na uaminifu kwa wateja na kwamba mamlaka haiko tayari kuona mawakala wanakiuka vigezo hivyo.

Kamishna huyo alizitaja baadhi ya sababu za kufutwa leseni kwa wakala huyo ni kushindwa kuwasilisha ada za bima zinazotokana na wateja kwa kampuni za bima na kusababisha upotevu wa fedha na usumbufu kwa wateja.

Kuhusu ukaguzi wa vyombo vya moto, alisema lengo ni kuhakikisha wamiliki wanakata bima bila shuruti ili kuepuka usumbufu na kusababisha ajali kwa wengine.

Alisema wamiliki wa vyombo vya moto wanakata bima kwa ajili ya vyombo vyao vinavyotembea barabarani ili kulinda usalama wa watu wingine wakiwamo wanaotumia barabara sambamba na kwenda na matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima namba 394 ya mwaka 2009.

"Tumezindua kampeni ya 'Kata Bima bila Shuruti' ambayo lengo lake kubwa ni kuona kwamba wamiliki wa vyombo vya moto wanakata bima kwa vyombo vyao kama sheria inavyowataka pamoja na kuwalinda na matukio ya ajali kwa wengine," alisema.

# Wakulima wataja kikwazo uzalishaji wa ngano

**Na Ashton Balaigwa, MBEYA**

WAKULIMA wa ngano wa Mikoa ya Mbeya na Njombe wamesema licha ya kunufaika na mbegu bora za zao la ngano, bado wanakabiliwa na ukosefu wa mashine za kulima na kuvunia pamoja na mbolea ya ruzuku ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Juzi, katika maonyesho ya wakulima, wafugaji na wavuvi ya Nanenane, wadau hao wa kilimo waliwasilisha changamoto hizo kwa watafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mjini Mbeya.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Safina kinachojishughulisha na kilimo cha ngano wilayani Makete, mkoani Njombe, Neema Jimsony, alisema licha ya kunufaika na mbegu zilizofanyiwa utafiti na TARI, kuna changamoto katika upatikanaji wa mashine za kilimo na kuvunia, hivyo kuathiri uzalishaji wa zao hilo.

"Mbegu tunazopata ni bora kabisa lakini tatizo ni miundombinu ya kilimo hasa katika mashine. Tunalazimika kufuata huduma hiyo umbali usiopungua kilomita 100. Sasa hii inaathiri uzalishaji kwa kuwa siyo wakulima wote wenye uwezo. Tunaomba serikali itusaidie," alisema Neema.

Mkulima wa zao hilo, Erasto Mwakitumbula kutoka Wilaya ya Mbeya Vijijini, aliomba serikali kuwapatia ruzuku ya mbolea kama inavyofanya katika mazao mengine ili kuongeza uzalishaji.

Akizungumzia mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema kwa sasa Tanzania inakusudia kufanya mageuzi katika kilimo cha ngano.

Alisema serikali inalazimika kutumia fedha za kigeni kuagiza wastani wa tani 900,000 za ngano kila mwaka kutoka nje kwa ajili ya matumizi ya ndani ili kukidhi mahitaji ya tani milioni moja. Uzalishaji wa ngano nchini ni tani 100,000 tu.

Alisema kupitia mkakati wake wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo, serikali imeipa jukumu TARI kuongeza uzalishaji wa mbegu za zao hilo ili kuwa na mashamba mengi katika mikoa mbalimbali nchini, hivyo kuokoa fedha za serikali kununua ngano kutoka nje ya nchi.

Dk. Mkamilo alisema tayari wameanza mikakati ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, Tanzania inajitegemea kwa kuzalisha ngano na kukidhi mahitaji ya ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi.

Alitaja mikakati hiyo ni pamoja na TARI kuzalisha mbegu za awali za kutosha za teknolojia ya kisasa ambazo zinahimili ukame na magonjwa ili kuzalishwa mbegu zilizothibitishwa ubora, ambazo zitatumika kwa wakulima wa zao hilo katika mikoa inayozalisha ngano na mikoa mingine mipya itakayofunguliwa.

Alisema kupitia mkakati huo, TARI itazalisha mbegu za awali tani 2,500 zitakazozalisha tani 50,000 za mbegu zilizothibitishwa ubora ambazo zitapandwa katika hekta 400,000 na kuwezesha kuzalisha zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka, hivyo kukidhi mahitaji ya ngano nchini. Mtafiti Mwandamizi wa Ngano nchini kutoka TARI Silian, Ismail Ngolinda, alisema tayari wamefanya utafiti kwa ajili ya kilimo hicho katika mikoa yenye joto na mvua chache ili kuongeza uzalishaji.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza katika uzinduzi wa maonyesho hayo juzi, alisema mpango uliopo sasa ni kuhakikisha ngano inalimwa kote nchini ili kuongeza uzalishaji.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Benki ya Azania, Augustino Matutu wakati alipotembelea maonyesho ya kimataifa ya wakulima Nanenane, jijini Mbeya jana. Azania ni wadhamini wakuu wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wadau soya wapeana mikakati kuongeza tija

**Na Mary Geofrey, MBEYA**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini (SAGCOT) kimekutana na wadau wa soya kujadili namna bora ya kuendeleza na kuongeza uzalishaji nchini ili kukidhi uhitaji wa soko la ndani.

Katika maonyesho ya Nanenane yanayoendelea kwenye Viwanja vya John Mwakangale, Mbeya, Mkuu wa Kongani na Maendeleo ya Ubia wa Ndani wa SAGCOT, Maria Ijumba, alisema jana kuwa kutokana na umuhimu wa zao hilo, kituo kimeona ni vizuri kuwakutanisha wadau toka sekta za umma na serikali.

"Katika kikao cha mazungumzo ya kisera tulijadili umuhimu wa kuandaa mkakati wa maendeleo ya soya nchini," alisema Ijumba na kuongeza kuwa sekta hiyo ndogo lazima ilete ushindani na matokeo chanya katika mnyororo wa thamani.

Alisema kikao kilijikita zaidi kuweka mkakati ambao utawezesha kuwaleta wabia katika utekelezaji ambao umehusishwa na kuratibiwa na wabia walioko katika mnyororo ili kuhakikisha zao hilo linamnufaisha mkulima.

Kwa mujibu wa Ijumba, kikao hicho kimewakutanisha wadau kutoka sekta binafsi, wadau wa maendeleo, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mratibu wa Utafiti Kitaifa, Mazao Jamii ya Mikunde wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Meshack Makenge, alisema kupitia kikao hicho wamejadili fursa za kumnufaisha mkulima mdogo na namna watakavyochagiza ukuaji wa sekta hiyo ndogo ya soya.

Alisema wameshazalisha aina tano za mbegu ambazo ni Uyole Soya 1, Uyole Soya 2, Uyole Soya 3, Uyole Soya 4 na aina kongwe ya mbegu Bossier. Kama zikitumiwa vizuri, tija yake ni kubwa kwa kuwa zinatoa mavuno mengi.

Mashaka Matafya kutoka kampuni ya uzalishaji wa mbegu ya soya ya Sange Agro Seed Ltd, alisema nchi imekuwa inaagiza soya kutoka nje na hivyo kupoteza fedha nyingi.

# Wanachama PSSSF watinga Nanenane kujua michango

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

WANACHAMA wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), wamekwenda katika Maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye Viwanja vya John Mwakangale, Mbeya, kujua hali uwasilishwaji wa michango yao.

Habiba Mhina, mwanachama wa PSSSF, alitembelea banda la PSSSF jana kupata taarifa za michango yake na baada ya kupatiwa huduma, alipongeza mfuko kwa kumpatia taarifa zake kwa haraka.

"Mimi ni mfanyakazi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, nimefika banda la PSSSF kupata taarifa za michango. Kwa kweli, chini ya dakika tano nimepata huduma na kukabidhiwa taarifa ya michango yangu," alisema.

Uongozi wa mfuko huo umesema maonesho ya mwaka huu ya Nanenane yana maslahi mapana kwake kutokana na uwekezaji ambao umefanywa katika maeneo ya kilimo na mifugo.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama, Bw. James Mlowe, katika banda la PSSSF kwenye maonesho hayo jana, alisema mfuko unayo majukumu manne ambayo ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.

Meneja huyo alisema PSSSF imewekeza katika Machinjio ya Kisasa Nguru wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, Kiwanda cha Kimataifa cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro (KLIC), akiitaja ni fursa kwa wafugaji.

Alisema wakulima na wafugaji ni wadau muhimu wa mfuko na kuwataka watembelee banda la PSSSF ili kujua fursa mbalimbali zinazopatikana katika mfuko kwa maeneo hayo ya uwekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo.

Akizungumzia kuhusu majukumu mengine ya msingi ya mfuko, Mlowe alisema PSSSF inatoa huduma kwa watumishi wa serikali kuu, serikali za mitaa na mashirika ambayo serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 30.

Akieleza zaidi ushiriki wa mfuko katika maonesho hayo, Mlowe alisema: "Hapa bandani ni ofisi kamili, tunatoa huduma kwa wanachama wetu kama ambavyo wanavyopata huduma katika ofisi zetu zilizopo nchi nzima Tanzania Bara na Zanzibar."

Alisema wanachama wakiwamo wastaafu wakitembelea banda hilo, watakutana na watumishi wanaojali mteja, waaminifu na wenye weledi na utayari wa kutoa huduma na watapata taarifa kuhusu michango, mafao yatolewayo na mfuko, uwekezaji na kuhakiki taarifa zao kwa njia ya alama za vidole (biometric).

Mhasibu Mkuu wa PSSSF, Grace Kabyemela, aliwahakikishia wanachama wakiwamo wastaafu kuwa mfuko uko katika hali nzuri na wanapata mafao yao kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

"Sheria inatutaka kuwa mwanachama anayestaafu anapowasilisha nyaraka zilizokamilika, anapaswa awe amelipwa mafao yake ya mkupuo ndani ya siku 60, lakini sisi PSSSF tumejiwekea malengo ndani ya siku 30 tunafanya malipo," alisema Grace.

Kuhusu malipo ya pensheni ya kila mwezi, Grace alisema mfuko unahakikisha ikifika tarehe 25 ya kila mwezi, wastaafu wanakuwa wamelipwa pensheni zao za mwezi.

# SINGIDA FOUNTAIN GATE YAKABIDHIWA BASI JIPYA

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Singida Fountain Gate juzi ilikabidhiwa basi jipya na benki ya NBC kwa ajili ya shughuli zake za kila siku kuelekea kwenye msimu mpya wa ligi kuu 2023/2024.

NBC imekabidhi basi hilo ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kutoa mikipo nafuu kwa klabu za ligi kuu Tanzania bara.

Singida Fountain Gate FC inakuwa klabu ya pili inayoshiriki ligi kuu kunufaika na mpango huo unaohusisha mkopo nafuu kutoka benki hiyo baada ya klabu ya KMC ya Dar es Salaam kunufaika pia na mpango huo Februari mwaka huu.

Hafla ya makabidhiano ya basi hilo lenye thamani ya Shilingi Milioni 470 imefanyika juzi kwenye Uwanja wa CCM Liti, Mkoani Singida muda mfupi kabla ya kuanza kwa tamasha la klabu hiyo la 'Singida Big Day'.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mkurugenzi wa Biashara wa hiyo, Elvis Ndunguru alisema basi hilo ni litasaidia shughuli za kila siku za klabu hiyo. ''Basi hili ni 'jipya kabisa la mwaka 2023, na limekatiwa bima na ambayo inahusisha usalama wa abiria wote ndani ya gari na bima hii inatumika kwa nchi za Africa Mashariki na kati (Comesa).Tunaamini litaisaidia sana timu hii katika safari zake wakati wa michezo ya ligi kuu kwa sababu linauwezo wa kubeba abiria 58," alisema Ndunguru.

Alisema ukosefu wa vyombo vya usafiri maalum kwa ajili ya timu zinazoshiriki ligi hiyo imekua ni moja ya chanzo cha vikwazo vingi katika gharama za uendeshaji na utendaji wa timu husika.

Kwa upande wake Rais wa Singida Fountain Gate, Japhet Makau pamoja kuishukuru benki hiyo kwa hatua hiyo kwa jitihada zake za kuiboresha ligi hiyo kimataifa alisema kuwa wamejipanga kuhakikisha mkopo huo unarejeshwa kwa wakati huku pia akiahidi kulitunza vyema basi hilo.

"Kupitia usafiri huu sasa tuna uhakika wa kusafirisha wachezaji wote na benchi la ufundi sambamba na mashabiki kwenda kwenye mechi zetu nje ya mkoa, hii ni hatua kubwa sana wenzetu wa NBC wametusaidia kuipiga," alisema Makau.

Alisema wataanza kulitumia basi hilo kwenye safari yao kuelekea Tanga kwenye mchezo wa ngao ya jamii dhidi ya Simba utakaochezwa Agosti 10 kwenye uwanja wa Mkwakani jijini humo.




Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru (kushoto) akimkabidhi funguo ya basi jipya Rais wa Klabu ya Singida Fountain Gate FC, Japhet Makau ikiwa ni sehemu ya mpango wa benki hiyo wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Hafla ya makabidhiano hayo yalifanyika juzi kwenye uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida wakati wa maadhimisho ya tamasha la klabu hiyo la 'Singida Big Day'. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Geita Gold, Parimatch mambo safi

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA zimebaki wiki mbili na siku tatu kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa ligi kuu, klabu ya Geita Gold imepata udhamini wa mwaka mmoja kutoka kampuni ya michezo ya kubahatisha ya Parimacth.

Mkataba huo ambao hata hivyo haukutajwa thamani yake, uliosainiwa jana kwenye ofisi za Halmashauri ya Jiji la Geita, unatarajiwa kusaidia timu hiyo katika shughuli za uendeshaji, usafiri na vifaa vya michezo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutiliana saini mkataba huo, Katibu wa klabu hiyo, Simon Shija, alishukuru kampuni hiyo kwa udhamini wao huo muhimu.

"Udhamini huu utatusaidia kurahisisha uendeshaji wa klabu na ushiriki wa mashindano mbalimbali pamoja na kuwa na tija kwa kuongeza thamani ya mpira wa miguu, tunaamini udhamini huu utachangia kwa kiasi kikubwa sisi kufanya vizuri kwenye ligi na kombe la FA, kwa kweli tunashukuru sana," alisema Shija.

Alisema kama klabu watahakikisha wanatimiza matakwa ya kimkataba waliyoingia na kampuni hiyo na wanaamini pia wadhamini wao hao watatimiza yote waliyokubaliana kwenye mkataba huo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald baada ya kusainiwa kwa mkataba huo alisema kampuni hiyo bado itaendelea kusaidia vilabu vingine vinavyoshiriki ligi kuu.

Gerald alisema mkataba huo walioingia na Geita Gold ni wenye faida kwa upande wa klabu hiyo katika kuelekea michuano ya Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza siku chache zijazo na umefungua pia milango ya ushirikiano na ligi nyingine ambazo Parimatch inadhamini kimataifa.

"Mkataba huu ni mwaka mmoja baina yetu na Geita Gold, lakini safari yetu haishii hapa Geita, tunaendelea kufanya mazungumzo na vilabu vingine vya Ligi Kuu na daraja la kwanza ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na bodi ya ligi ili kuhakikisha ligi ya Tanzania inakuwa na hadhi kubwa", alisema Gerald.

Alisema lengo lao kama kampuni ni kusaidia ustawi wa ligi za soka hapa nchini na kuunga mkono juhudi za TFF na serikali kwa ujumla kwa kusaidia kuinua michezo hapa nchini.

Alisema Parimatch imekuwa ikifanya kazi nchini tangu mwaka 2019, ikitoa huduma mbalimbali ikijumuisha malipo ya haraka, odds kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, kasino na michezo ya 'virtual'.

Mbali na soka, kampuni ya Parimatch pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye mchezo wa tenisi, UFC, mpira wa kikapu, kriketi na mpira wa magongo.

## Kagera Sugar yafungwa, yapozwa na msosi Uganda

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar juzi ilianza vibaya ziara yao nchini Uganda kwa kuchapwa mabao 2-1 na Vipers FC katika uwanja wa St Mary's Katende jijini Kampala na baada ya hapo wakafanyiwa hafla kubwa kwa kuandaliwa chakula cha jioni na wenyeji wao hao.

Kagera Sugar kwa sasa ipo kwenye 'pre season' ikijiandaa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo waliamua kwenda kujipima nguvu Uganda.

Vipers FC nayo inajiandaa kwa michuano mbalimbali ikiwemo Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo itanzia hatua za awali kwa kucheza na Jwaneng Galaxy ya Botswana Agosti 18.

Wenyeji walitangulia kupata bao la kwanza dakika ya 27 lililowekwa wavuni na Abdul Lumala kabla ya straika Mbrazi Giancarlo Rodriguez kupachika bao la pili dakika ya 67.

Hamisi Kiiza ambaye alikuwa anacheza nyumbani kwao, ndiye aliyeifungia Kagera Sugar bao la kufutia machozi kwa mkwaju wa penalti dakika ya 76.

## Simbu apania medali riadha dunia

**Na Abdallah Mataka**

MWANARIADHA wa kimataifa wa Tanzania, Alphonce Simbu amesema amepania kutwaa medali ya dhahabu kwenye mashindano ya dunia ya riadha yatakayofanyika Budapest, Hungary kuanzia Agosti 19-27 mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe kutoka Arusha alipoweka kambi, Simbu alisema amepania kuweka rekodi ya kuwa Mtanzania wa kwanza kutwaa medali ya dhahabu katika mashindano hayo ya dunia.

"Naendelea vizuri na mazoezi ya maandalizi ya mashindano hayo hapa Arusha chini ya kocha wangu Anthony Muingereza, nina matumaini makubwa ya kufanya vizuri katika mashindano ya dunia, lengo langu kuu ni medali ya dhahabu na hilo linawezekana"alisema Simbu.

Simbu aliwahi kushinda medali ya shaba katika mashindano hayo mwaka 2017 yalipofanyika jijini London, Uingereza .

Mwanariadha huyo ndiye mwakilishi pekee wa Tanzania katika mashindano hayo baada ya mwanariadha mwingine wa kimataifa, Gabriel Geay kuomba kujitoa ili kushiriki mashindano mengine.

Mwanariadha huyo ambaye amekuwa akifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa, alisema kwa sasa amekuwa akifanya mazoezi kwa gharama zake bila msaada wowote kutoka Shirikisho la Riadha Tanzania (RT).

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MBAPPE AITAKA CHELSEA**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, ameiambia Chelsea kwamba yuko tayari kujiunga nao kutoka Paris St Germain kwa mkataba wa mwaka mmoja ikiwa ataruhusiwa kuhamia Real Madrid kwa uhamisho wa bure msimu ujao. **(Sport)**

**MAN YAJITOSA KWA LAVIA**
KLABU ya Manchester United imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa Southampton na Ubelgiji, Romeo Lavia baada ya ombi la Liverpool kukataliwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. **(Independent)**

**HOJLUND NA MAN**
UTHIBITISHO wa Manchester United wa kumsajili mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund kutoka Atalanta unaweza kucheleweshwa hadi wikiendi baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kuwasili kwa kuchelewa. **(Manchester Evening News)**

**KANE AITAKA BAYERN**
MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30 yuko tayari kutoa sehemu kubwa ya mshahara wake pale Tottenham Hotspur ili kusaidia kuhamia Bayern Munich. **(Bild)**

**MICKY KUTUA SPUR**
TOTTENHAM Hotspur inakaribia kumsajili mlinzi wa Wolfsburg, Micky van de Ven baada ya kuafikiana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. **(Talksport)**

**TOMIYASU KUTUA INTER**
INTER Milan imepanga kumleta mlinzi wa Arsenal, Takehiro Tomiyasu mwenye umri wa miaka 24 katika klabu hiyo. **(Gazzetta dello Sport)**

**CANCELO AWANIWA BARCA**
BARCELONA wako kwenye mazungumzo na Manchester City kuhusu kumnunua beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo umri wa miaka 29. **(Talksport)**

**DE BEEK KUUZWA**
KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo na Real Sociedad kuhusu mauzo ya kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri 26, ambayo yatasaidia kufadhili uhamisho wa kiungo wa kati wa Fiorentina mwenye umri wa miaka 26 wa Morocco, Sofyan Amrabat. **(Mail)**

**CAICEDO NA CHELSEA**
CHELSEA inakabiliwa na ushindani katika usajili wa kiungo wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo huku klabu ambayo bado haijatambulika ikivuka dau la pauni milioni 80 la The Blues hao kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. **(Athletic)**

**VILLA YAMTAKA ADAMS**
ASTON Villa imejiunga katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Leeds United, Tyler Adams mwenye umri wa miaka 24 kwa pauni milioni 25. **(Mail)**

**JAMES AOTA MBAWA**
KLABU ya West Ham inatafuta mbadala wa kiungo wa kati wa Southampton, James Ward-Prowse baada ya dau la pauni milioni 30 la kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kukataliwa. **(Sky Sports)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JESUS KUKOSA MWANZO WA MSIMU MPYA

NI baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti utakaomuweka nje kwa wiki kadhaa, Kocha Arteta asema...

**LONDON, England**

STRAIKA wa Arsenal, Gabriel Jesus atakuwa nje ya dimba 'kwa wiki chache' baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti, bosi wa washikabunduki hao, Mikel Arteta amethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 aliukosa mchezo wa Jumatano wa ushindi kwenye kombe la Emirates dhidi ya Monaco, ambapo Arsenal walishinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya sare ya 1-1 London Kaskazini.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Arteta alithibitisha Jesus amekuwa akisumbuliwa na goti tangu msimu uliopita, wakati alipokosekana kwa miezi baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti alipoumia Desemba kwenye michuano ya Kombe la Dunia akiwa na Brazil kule Qatar.

"Bahati mbaya, ameumia tena," alisema Arteta.

"Alikuwa na tatizo katika goti ambalo limekuwa likimsumbua mara kadhaa. Sio jambo kubwa lakini anaonekana kuwa nje kwa wiki chache nadhani."

"Ni pigo kubwa kwa sababu tulimrudisha katika ubora wake, hasa jinsi alivyocheza dhidi ya Barcelona (jijini Los Angeles Jumatano iliyopita), na alikuwa katika hali nzuri na tukampoteza."

"Lakini amekuwa akihisi usumbufu wiki chache zilizopita na ilibidi tuliangalie, tulilazimika kufanya uamuzi na bora zaidi ni kumlinda mchezaji na kumrudisha haraka iwezekanavyo kwa hiyo tuliamua kufanya hivyo."

"Ni jambo linalohusiana na jeraha la awali alilokuwa nalo na upasuaji. Alikuwa na muwasho kwenye goti na ilibidi tulitatue."

Arsenal wataanza msimu huu na Eddie Nketiah na Folarin Balogun, ambaye anahusishwa na kuondoka katika klabu hiyo.

"Mipango na Flo haibadiliki hata kidogo lakini kwa bahati mbaya na Gabby hatutakuwa naye," aliongeza Arteta.

"Tuna chaguzi zingine za kucheza na sifa tofauti za wachezaji na tutabadilika."

Arsenal itamenyana na Manchester City katika mchezo wa Ngao ya Jamii Jumapili Uwanja wa Wembley kabla ya mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu ya England Agosti 12 wakiwa nyumbani dhidi ya Nottingham Forest.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8

MECHI KALI
SHEFFIELD WED
VERSUS
SOUTHAMPTON
1 | 3.06
X | 3.26
2 | 2.19

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN CITY YAMALIZANA NA GVARDIOL

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imekubali kufanya makubaliano na RB Leipzig kumsajili beki Josko Gvardiol, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wamepanga kulipa ada ya euro milioni 90 moja kwa moja, na makubaliano hayo hayajumuishi nyongeza.

Gvardiol mwenye umri wa miaka 21 atafanyiwa uchunguzi wa kiafya na anatarajiwa kusafiri hadi England mara moja.


Kuna uwezekano mkubwa wa kucheza mechi yake ya kwanza katika Ngao ya Jamii Jumapili dhidi ya Arsenal huko Wembley, lakini anafaa kusajiliwa kwa wakati ili kupatikana kwa mechi ya ufunguzi wa ligi ya City dhidi ya Burnley pale kwenye uwanja wa Turf Moor, Agosti 11.

Hapo awali Leipzig walikuwa wamemthaminisha Gvardiol kwa euro milioni 100, msimamo ambao ulizuia mazungumzo mapema msimu huu wa joto.

Thamani ya Leipzig ingemfanya Gvardiol kuwa beki ghali zaidi duniani, lakini ada ya mazungumzo ya City ni chini ya pauni milioni 80 ambayo Manchester United ililipa Leicester City kwa Harry Maguire mwaka 2019.

Gvardiol atakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Pep Guardiola majira haya ya joto baada ya kuwasili kwa Mateo Kovacic kutoka Chelsea.

Ilkay Gündogan na Riyad Mahrez wote wameondoka, na bado kunaweza kuwa na wachezaji wengine wanaomaliza muda wao, wakiwemo Bernardo Silva, Kyle Walker, Kalvin Phillips na Aymeric Laporte.



# Buffon astaafu soka na miaka 45

**ROME, Italia**

GOLIKIPA mkongwe Gianluigi Buffon amestaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 45.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2006 alikaa msimu uliopita katika klabu ya utotoni Parma akisaidia kumaliza katika nafasi ya nne kwenye Serie B na kufika hatua ya 16 bora ya Coppa Italia, ambapo walitolewa na washindi mabingwa, Inter Milan.

Buffon alitia saini nyongeza ya mkataba wake na I Crociati hao hadi 2024, lakini ameamua kuachana nayo kabla ya msimu wa 2023-24.

Mlinda mlango huyo wa Italia alishinda Kombe la UEFA mwaka msimu wa 1998-99 katika kipindi chake cha kwanza akiwa na Parma kabla ya kuhamia Juventus Julai 2001 kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia kwa mlinda mlango ya pauni milioni 32.

Alifurahia mafanikio makubwa akiwa na Bianconeri, na kutwaa taji la Serie A mara 10 kwa vipindi viwili akiwa na kikosi cha Turin na kucheza mechi 685 kwa jumla.

Juventus iliandika kwenye tovuti yao rasmi: "Leo (jana) ni siku ya kila mtu kufikiria nyuma kuokoa mvuto wako, jinsi ulivyovuka historia, kuwaaga wachezaji wa ajabu na kuona kuibuka kwa warithi wao, huku ukiwa umebaki mahali.

"Ulionesha uthabiti na kutegemewa kwa bingwa ambaye tabasamu lake lingeweza kuondoa woga wowote na kuwajaza wafuasi na wachezaji wenzako hisia kwamba ulikuwa mtu asiyeweza kuvunjika moyo.

"Ulitupa sababu ya kuota na ukafanya ndoto hizo kuwa kweli. Leo ni mwisho wa enzi na tunaheshimika sana kuishi maisha haya. Sisi ni sehemu ya hadithi yako na wewe ni sehemu yetu.

"Asante, Gigi! Tunakutakia kila la kheri katika maisha mengine ya baadaye."

Buffon alitumia msimu wa 2018-19 kule Paris Saint-Germain, akiongeza taji lingine la ligi kwenye mkusanyiko wake.

Pia alishinda tuzo nyingi binafsi wakati wake wa uchezaji, ikiwa ni pamoja na tuzo 13 za Kipa Bora wa Mwaka wa Serie A.

Nyota huyo wa Italia anashika nafasi ya tisa kwenye orodha ya wachezaji wa kiume waliocheza mechi nyingi za kimataifa baada ya kufikisha mechi 176 katika kipindi cha miaka 23 akiwa na Azzurri.

359,317/-

# SINGIDA FG, SPORTPESA WATEMBELEA WAGONJWA

**Na Julieth Ng'oma, Turdaco**

KLABU ya Singida Fountain Gate pamoja na wadhamini wao kampuni ya Sportpesa juzi walitoa misaada mbalimbali kwa akina mama wajawazito kwenye hospitali ya Mkoa wa Singida.

Misaada hiyo ilitolewa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya tamasha la klabu hiyo la 'Singida Big Day' iliyofanyika juzi kwenye uwanja wa CCM Liti mkoani humo.

Akizungumza kwenye ziara hiyo hospitalini hapo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Sportopesa, Tarimba Abbas, alisema kama wadhamini wa klabu hiyo wanaunga mkono katika matukio yao mbalimbali hasa ya kurudisha kwa jamii sehemu ya kile walichokipata.

"Kilichofanya tuwe hapa ni kwa sababu ya Singida Fountain Gate FC tukiwa sisi ndio wadhamini wao wakuu tunaungana nao katika kutatia moyo wagonjwa mbalimbali, hili ni jambo jema, kurudisha kidogo wanachokipata kwa jamii," alisema Tarimba.

Alisema kama wadhamini wataendelea kushirikiana na klabu hiyo katika matukio mbalimbali ya kijamii.

Kwa upande wake, Rais wa klabu hiyo Japhet Makau, aliishukuru Sportpesa kwa udhamini wao lakini kwa kushirikiana nao kutoa misaada hiyo.

Aidha, Mganga Mkuu wa Hospital hiyo Victorina Ludovick alishukuru uongozi wa Singida FG na Sportpesa kwa msaada wao kwani wameonyesha moyo wa kujali akisema "nimefurahi sana kwani nimejua mnatambua umuhimu wa Wanasingida na asanteni sana kwa kuja kututembelea na kutupa moyo."

Ludovick alisema anaitakia kila la heri klabu hiyo iweze kufanya vizuri kwenye mashindano itakayoshiriki.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Sportpesa, Tarimba Abass (kulia) akikabidhi misaada mbalimbali kwa uongozi wa hospitali ya Mkoa wa Singida juzi. **PICHA: SPORTPESA**

## Yanga sc yatamba kufanya makubwa

INATOKA UK. 24

go kubwa ni kutunza kumbukumbu kwa kizazi kijacho kutokana na kile tulichokutana nacho," alisema Kamwe

Meneja huyo wa Habari, alisema ndani ya filamu hiyo pia wataonyesha kila kitu katika safari zao za ndani na nje ya nchi mpaka kufikia mafanikio waliyoyapata.

Aidha, Mkurugenzi wa wanachama wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa alisema wameandaa utaratibu maalumu kwa ajili ya kuwaalika watu katika uzinduzi huo.

# Shime: Huu ni mchezo wa fainali

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya taifa ya soka ya wasichana chini ya miaka 18, Bakari Shime amesema mchezo wa leo dhidi ya Uganda ni kama fainali kwao kwa kuwa ni ushindi tu unaotakiwa ili kujitangaza mabingwa wa michuano ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Leo Tanzania na Uganda ambazo zote zina pointi tisa zinaumana kwenye mchezo wa mwisho wa michuano hiyo kwenye uwanja wa Azam Complex na mshindi atakuwa amejihakikishia kutwaa ubingwa huo kwa mwaka huu.

Juzi Uganda ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Burundi na kufikisha pointi tisa sawa na Tanzania huku zote zikiwa zimecheza michezo mitatu.

Shime alisema mchezo huo wa leo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu wote wana alama sawa na kila mmoja anahitaji ushindi katika mechi ya mwisho.

Alisema anaimani kuwa ana kikosi bora katika mashindano hayo lakini hawataidharau Uganda kwa sababu inawapa ushindani miaka yote kila wanapokutana.

"Mechi ni ngumu kwa sababu ya upinzani wetu lakini hatuhitaji kuona kombe linaondoka hapa kwetu, tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo wetu huo na kutwaa ubingwa wa michuano hii.

"Kama nilivyosema awali kuwa baada ya mechi na Zanzibar nina kibarua kingine kigumu dhidi ya Uganda ambapo kwetu ni fainali na tumejiandaa vizuri kushinda," alisema Shime. Aliongeza kuwa anaamini wachezaji wake watafanya vizuri kwenye mchezo huo kwa kuwa amefanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye michezo iliyopita.

Tanzania ilianza mashindano hayo kwa kuwafunga Burundi mabao 3-0, kisha wakainyoa Ethiopia mabao 2-0 na kuwapiga bao 1-0 ndugu zao Zanzibar.

Wakati Uganda wao walianza kwa kuwaadhibu Ethiopia bao 1-0, wakawanyuka Zanzibar mabao 3-0 na kuwabutua Burundi mabao 7-0.

Kwa matokeo ya timu zote kwenye mechi zilizopita, Tanzania inahitaji zaidi ushindi kutwaa ubingwa huo kwa kuwa wamezidiwa na Uganda mabao matano katika idadi ya magoli ya kufunga.

Kulingana na msimamo, tayari Ethiopia wenyewe wamejihakikishia nafasi ya tatu kwenye mashindano hayo ya mwaka huu huku Zanzibar na Burundi zenyewe zitashika nafasi ya nne na tano.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 04/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3711 | Gwangju vs Daejeon Citizen | 2.11 | 3.23 | 3.07 |
| 13:30 | 5589 | FC Seoul vs Pohang Steelers | 2.26 | 3.19 | 2.83 |
| 14:35 | 3802 | Beijing Guoan vs Henan Jianye | 1.46 | 4.13 | 5.44 |
| 15:00 | 5824 | PSS Sleman vs Persija Jakarta | 3.52 | 3.42 | 1.87 |
| 17:00 | 1716 | FC Obolon Kiev vs Dynamo Kiev | 11.14 | 5.67 | 1.18 |
| 18:00 | 1267 | FC Andijon vs Surkhon Termez | 2.25 | 2.98 | 3.03 |
| 18:00 | 3154 | FC Spaeri-Dinamo vs 2 Tbilisi | 1.72 | 3.98 | 3.72 |
| 18:00 | 3363 | Ilves Tampere vs Haka | 2.11 | 3.23 | 3.07 |
| 18:00 | 5057 | FK Babrungas Plunge vs FK Panevezys B | 1.62 | 3.88 | 4.23 |
| 18:30 | 1252 | Hifk vs Kapa | 1.58 | 4.13 | 4.23 |
| 19:00 | 1339 | SK Hranice vs Fastav Zlin B | 2.69 | 3.35 | 2.33 |
| 19:00 | 3182 | Jagiellonia vs Widzew Lodz | 2.33 | 3.07 | 2.82 |
| 19:00 | 3608 | Blansko vs FC Slovan Rosice | 3.67 | 3.72 | 1.79 |
| 19:00 | 4667 | Flora Tallinn vs Kuressaare | 1.22 | 5.70 | 9.37 |
| 19:00 | 5009 | AL Aqaba vs Sahab Club | 2.34 | 3.00 | 2.95 |
| 19:00 | 5998 | Suduva vs FM Auska Alytaus | 2.53 | 3.14 | 2.53 |
| 19:10 | 1233 | Dornbirn vs Liebherr Gak | 3.71 | 3.71 | 1.78 |
| 19:10 | 4635 | SV Horn vs FC Liefering | 2.89 | 3.65 | 2.08 |
| 19:10 | 5509 | SKN St Polten vs SV Lafnitz | 1.67 | 3.82 | 4.18 |
| 19:30 | 1620 | Paderborn vs Osnabruck | 1.64 | 4.01 | 4.51 |
| 19:30 | 1986 | Hertha BSC vs Wehen | 1.55 | 4.11 | 5.21 |
| 20:00 | 2381 | Horsens vs HB Koge | 1.66 | 3.48 | 4.53 |
| 20:00 | 3415 | FC Krasnodar vs Nizhny Novgorod | 1.61 | 3.70 | 5.03 |
| 20:00 | 3889 | Silkeborg vs Vejle BK | 1.70 | 3.66 | 4.72 |
| 20:00 | 3945 | Slavia Mozyr vs FC Minsk | 2.01 | 3.16 | 3.51 |
| 20:00 | 4725 | Hillerod vs Hobro | 2.58 | 3.34 | 2.37 |
| 20:00 | 5341 | Skeid Fotball vs Fredrikstad | 3.32 | 3.42 | 1.93 |
| 20:30 | 1394 | Sekhukhune United vs Mamelodi Sundowns | 5.34 | 3.39 | 1.64 |
| 20:30 | 2354 | FC Thun vs FC Baden | 1.58 | 3.75 | 4.76 |
| 21:00 | 4360 | Lokomotiva Zagreb vs Vsnk Varazdin | 1.69 | 3.63 | 4.14 |
| 21:00 | 4890 | Puskas Akademia vs Ujpest FC | 1.76 | 3.56 | 3.97 |
| 21:00 | 5000 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.10 | 3.37 | 3.06 |
| 21:15 | 4641 | NK Aluminij vs Luka Koper | 2.88 | 3.13 | 2.25 |
| 21:15 | 4714 | FC Sion vs AC Bellinzona | 1.30 | 5.04 | 7.05 |
| 21:15 | 4721 | FC Schaffhausen vs FC Wil | 2.82 | 3.33 | 2.20 |
| 21:30 | 1505 | Josko Ried vs Admira Wacker | 1.81 | 3.67 | 3.62 |
| 21:30 | 1603 | Ruzomberok vs MFK Skalica | 1.87 | 3.23 | 3.78 |
| 21:30 | 2555 | Wisla Plock vs Lechia Gdansk | 1.79 | 3.52 | 3.73 |
| 21:30 | 2888 | LKS Lodz Pss vs Korona Kielce | 2.33 | 3.07 | 2.82 |
| 21:30 | 4902 | Universitatea Craiova vs Hermanstadt | 1.68 | 3.59 | 4.61 |
| 21:30 | 4997 | Wihdat Amman vs Al Ahli Amman | 1.65 | 3.15 | 5.69 |
| 21:45 | 1954 | Bohemians FC vs Drogheda Utd | 1.67 | 3.63 | 4.23 |
| 21:45 | 1984 | Waterford Utd vs Kerry FC | 1.03 | 10.07 | 27.18 |
| 21:45 | 2617 | Arbroath vs Dundee Utd | 3.98 | 3.73 | 1.74 |
| 21:45 | 2721 | Standard Liege vs Union Saint Gilloise | 3.08 | 3.42 | 2.14 |
| 21:45 | 4213 | Sligo Rovers vs St Patricks | 2.86 | 3.16 | 2.25 |
| 21:45 | 5435 | Cobh Ramblers vs Wexford Youths | 1.96 | 3.53 | 3.17 |
| 21:45 | 5446 | Coleraine FC vs Ballymena Utd | 1.37 | 4.32 | 6.83 |
| 22:00 | 2392 | Finn Harps vs Galway United | 11.17 | 6.09 | 1.17 |
| 22:00 | 4547 | Sheffield Wed vs Southampton | 3.06 | 3.26 | 2.19 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Agosti 4, 2023
Nipashe



Jesus kukosa mwanzo wa msimu mpya UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga, Mudathir Yahya(katikati) akiwania mpira na Khalid Aucho(kushoto) wakati wa mazoezi ya timu hiyo jana kwenye viwanja vya Avic Town Kigamboni, wengine ni Farid Mussa na Gift Fred. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC YATAMBA KUFANYA MAKUBWA

●●● Yawahakikishia mashabiki kuona kiwango bora zaidi ya kile walichokiona siku ya Mwananchi, kuzindua filamu maalum ikionyesha.....

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

ZIKIWA zimebakia wiki mbili kabla ya kuanza kwa msimu mpya, uongozi wa Yanga umewahakikishia mashabiki wa timu hiyo kuwa timu yao ipo imara na wataona makubwa zaidi huku wakijiandaa kuzindua filamu yao maalum.

Uongozi wa klabu hiyo umesema kile kilichoonekana kwenye mchezo wao wa kirafiki katika kilele cha tamasha la mwananchi dhidi ya Kaizer Chief ni sehemu tu ya ubora wa kikosi chao msimu huu.

Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison amesema walichokiona wanachama na mashabiki wa Yanga siku ya Mwananchi basi watarajie kuona makubwa zaidi kwani wachezaji hao wanaonekana kuwa na vitu vya ziada mazoezini.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga wategemee kikubwa zaidi ya kile kilichoonekana Siku ya Mwananchi, kila siku zinavyozidi kwenda wachezaji wanaonyesha mambo ya ziada mazoezini na kumfanya kocha wetu Miguel Gamondi kuwa na matumaini ya kufanya vizuri, mashabiki hawajaviona vitu vingi kutoka kwa wachezaji wetu wapya, nawahakikishia wataendelea kufurahi msimu huu mpya," alisema Walter.

Aidha, alisema usajili wa wachezaji wao wa kimataifa ulikuwa wa 'kisayansi' na si wa kukurupuka.

"Sidhani kama kuna mtu anatakiwa kuwa na wasiwasi na wachezaji wapya wa Yanga kwa sababu wameshawaona vijana wao jinsi wanavyocheza uwanjani siku ya Mwananchi, usajili unaofanyika hapa haufanyiki kwa kujaza nafasi au ili mradi, tumefanya usajili kwa mahitaji ya timu na ubora wa timu yetu, sasa niseme tu kile ambacho wameshakiona siku ile pale kwa mkapa (Uwanja wa Benjamin Mkapa) ni mwanzo tu, mambo bado," alisema Walter.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo unatarajia kuzindua filamu fupi ikielezea mapito yao msimu uliopita.

Filamu hiyo fupi itaangazia changamoto walizokutana nazo tangu kuanza kwa msimu 2022/2023 pamoja na yale waliyokutana nayo kwenye mashindano ya kimataifa.

Afisa habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe alisema uzinduzi wa filamu hiyo utafanyika Dar Free Market kwa mialiko maalum.

"Filamu hii tumeshirikiana na wataalamu mbalimbali wa tasnia ya filamu na len-

UKURASA. 23

## Simba: Hatutaacha kitu msimu huu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umesema msimu huu hawataacha kombe lolote kwenye mashindano ya ndani watakayoshiriki na wamejipanga kufika angalau nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema malengo yao makubwa ni kufanya vizuri katika kila mashindano watakayoshiriki.

Alisema wanamatarajio hayo kwa sababu ya aina ya wachezaji waliowasajili watawasaidia kufikia malengo yao ya kutwaa mataji yote ya ndani na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tumefanya usajili mzuri, matumaini yetu msimu huu ni kuchukuwa mataji yote ya ndani lakini pia kufika hatua ya nusu fainali ya ligi ya Mabingwa Afrika, kwa ubora wa wachezaji tuliowasajili na wale waliopo tuna uhakika wa kufika malengo hayo" alisema Ahmed na kuongeza,

"Kwa hapa nyumbani hakuna tutakachokiacha kila kilichopo mbele yetu tutabeba, tutaanza na ngao ya jamii," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine, kuelekea kwenye tamasha la Simba Day, uongozi wa klabu hiyo umemtangaza staa wa muziki wa kizazi kipya nchini, Ally Kiba kuwa ndiye atakuwa mtumbuizaji mkubwa katika tamasha hilo litakalofanyika keshokutwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema waliangalia msanii ambaye anapendwa na watu wengi, wakaamua kumthamini kwa kumkaribisha katika klabu hiyo.

"Tunajua kuwa Ali Kiba ni msanii mkubwa Afrika, tunaamini kwa kufanya nae kazi atakuwa balozi mzuri wa klabu yetu katika mataifa mbalimbali ambayo anakwenda kufanya kazi," alisema Kajula.

Aidha, Kiba kwa upande wake anawashukuru Simba kwa kutambua thamani yake na anaamini atakuwa na furaha akiwa hapo kutokana na rekodi nzuri walizonazo katika mashindano mbalimbali.

"Nimepata mapokezi makubwa Simba, moyo unapenda unapo thaminika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >